JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI WA HESABU ZA SERIKALI

RIPOTI ZA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI (CAG) KWA MWAKA WA FEDHA 2019/20

TOLEO MAALUMU LA MWANANCHI

www.nao.go.tz

" Kila raia anayo haki ya kupewa taarifa wakati wote kuhusu matukio mbalimbali nchini na duniani kote ambayo ni muhimu kwa maisha na shughuli za mwananchi "

Ibara ya 18 (2)

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI WA HESABU ZA SERIKALI

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi,
Jengo la Ukaguzi, Mtaa wa Hazina, S.L.P 950, 41104 Dodoma, Tanzania
Simu:+255 (26) 2321759, Nukushi: +255 (26) 2321245
Barua pepe: ocag@nao.go.tz | Tovuti: www.nao.go.tz

RIPOTI ZA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/20

TOLEO MAALUMU LA MWANANCHI

YALIYOMO

UJUMBE WA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI 1

MUHTASARI 3

SURA YA KWANZA 5

1.0 UTANGULIZI 5

SURA YA PILI 11

2.0 MAELEZO YA JUMLA KUHUSU UKAGUZI NA HATI ZA UKAGUZI WA TAARIFA ZA FEDHA 11

SURA YA TATU 15

3.0 UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI 15

SURA YA NNE 18

4.0 RIPOTI YA UKAGUZI WA HESABU ZA SERIKALI KUU KWA MWAKA 2018/19 18

SURA YA TANO 29

5.0 RIPOTI YA UKAGUZI WA HESABU ZA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA.. 29

SURA YA SITA 47

6.0 RIPOTI YA UKAGUZI WA HESABU ZA MASHIRIKA YA UMMA..................... 47

SURA YA SABA.. 64

7.0 RIPOTI YA UKAGUZI WA HESABU ZA MIRADI YA MAENDELEO 64

SURA YA NANE.. 77

8.0 RIPOTI ZA UKAGUZI WA UFANISI 77

SURA YA TISA 93

9.0 UTEKELEZAJI WA SERA YA TAIFA YA TEHAMA NA MKAKATI WA SERIKALI MTANDAO 93

"Ni Imani yangu kuwa taarifa hizi zitakuwa chachu ya uwajibikaji kwa makundi yenye dhamana ya kuhakikisha kwamba tija na ufanisi vinakuwa sehemu ya kila mwenye dhamana ya kusimamia rasilimali za Umma."

Charles E. Kichere

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali

UJUMBE WA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

Ninayo furaha kwa mara nyingine kukitambulisha kitabu cha Toleo Maalumu kwa ajili ya Mwananchi, kwa msomaji wangu.

Kwa kuzingatia matakwa ya kikatiba, kisheria na kitaaluma, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAOT) imekuwa kila mwaka ikiandaa kitabu hiki mara baada ya Ripoti za Ukaguzi kutoka kwa mwaka husika. Lengo kuu likiwa ni ushirikishwaji wa wananchi katika mchakato wa kaguzi mbalimbali zinazofanywa na Ofisi yangu pamoja na matokeo yake.

Dhima kuu ya kitabu hiki ni kuwa chachu miongoni mwa wananchi katika kujijengea tabia ya ufuatiliaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo zinazotekelezwa na Serikali.

Nia yangu ni kuendelea kushirikisha jamii na wadau mbalimbali katika kufanikisha majukumu niliyonayo kikatiba katika kuhakikisha kuwa Rasilimali za Taifa zinahifadhiwa na kutumiwa vizuri kwa kufuata taratibu na kanuni za utawala bora ili kuhakikisha maendeleo yanapatikana kwa wananchi.

Toleo hili linatoa taarifa za matokeo ya kikaguzi yaliyowasilishwa katika ripoti kuu saba kama ifuatavyo:

i. Ripoti ya Ukaguzi ya Serikali Kuu;
ii. Ripoti ya Ukaguzi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa;
iii. Ripoti ya Ukaguzi ya Mashirika ya Umma;

iv. Ripoti ya Ukaguzi ya Miradi ya Maendeleo;
v. Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi;
vi. Ripoti ya Ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA;
vii. Ripoti ya ufuatiliaji wa mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti za Ukaguzi wa ufanisi kwa miaka iliyopita;

Ni imani yangu kuwa taarifa hizi zitakuwa chachu ya uwajibikaji wa makundi yenye dhamana ya kuhakikisha kwamba tija na ufanisi vinakuwa sehemu ya kila mwenye dhamana ya kusimamia rasilimali za umma.

Ninapenda kuwashukuru wote walioshiriki katika kuandaa Toleo hili, hasa wafanyakazi wa Ofisi yangu ambao wamehakikisha toleo hili linapatikana kwa wakati. Pia, napenda kuwahimiza wananchi wote kusoma toleo hili kwani watafahamu kwa kina kazi zinazofanywa na Ofisi yangu pamoja na matokeo ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Charles E. Kichere
Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

Agosti 2021

MUHTASARI

Kitabu hiki kinatoa sura ya Ripoti za Hesabu za Serikali, pia kimegawanyika katika sura kuu tisa zinazowasilisha taarifa za Fedha zilizokaguliwa kwa hesabu zinazoishia tarehe 30 Juni 2020 pamoja na ukaguzi wa Ufanisi.

Sura ya Kwanza: Inatoa taarifa ya utangulizi wa kijitabu hiki, Mamlaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Majukumu ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi na wadau mbalimbali wanaofanya kazi na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kama vile Bunge.

Sura ya Pili: Sura hii inatoa maelezo kuhusu kaguzi mbalimbali,aina ya hati na tafsiri zake, idadi ya hati zilizotolewa kwa kaguzi za Serikali za Mitaa, Serikali Kuu, mashirika ya Umma, Miradi ya Maendeleo, Ufanisi na Ukaguzi wa Tehama.

Sura ya Tatu: Sura hii inaonyesha utekelezaji wa Mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti za kipindi kilichopita katika ukaguzi wa hesabu za Serikali.

Sura ya Nne: Sura hii inatoa muhtasari wa Ukaguzi wa Serikali Kuu ambayo inajumuisha wizara, idara na wakala wa Serikali.

Sura ya Tano: Sura hii inatoa taarifa za ukaguzi wa hesabu za Serikali za Mitaa ambayo inajumuisha ukaguzi wa taarifa za Halmashauri za Wilaya, Manispaa, Miji na Mijiji.

Sura ya Sita: Sura hii inahusu muhtasari wa majumuisho ya matokeo ya ukaguzi wa Mashirika ya Umma kwa mwaka ulioishia Mwaka 2019.

Sura ya Saba: Sura hii inatoa muhtasari wa Ripoti za Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo, mfano mradi wa Umeme wa Julius Nyerere na Reli ya kisasa (SGR).

Sura ya Nane: Sura hii inatoa taarifa za kaguzi za ufanisi kwa mwaka ulioishia 30 Juni 2020.

Sura ya Tisa: Sura hii inatoa muhtasari wa baadhi ya mapungufu yaliyobainika utengenezaji, uendeshaji na usimamizi wa mifumo ya Tehama katika taasisi na idara za Serikali zilizokaguliwa katika mwaka wa fedha 2019/2020.

SURA YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni Taasisi kuu ya ukaguzi yenye jukumu la kufanya ukaguzi wa mapato na matumizi ya Serikali, kama yanavyoidhinishwa na Bunge na kutoa taarifa ya ukaguzi Bungeni. Ofisi hii inaongozwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambaye majukumu yake yameainishwa wazi katika Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 (kama ilivyorekebishwa mara kwa mara); Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya Mwaka 2008 na Kanuni zake za Mwaka 2009, pamoja na Sheria nyingine ikiwemo Sheria ya Fedha za Umma ya Mwaka 2001; na Sheria ya Serikali za Mitaa Na. 9 ya Mwaka 1982 (iliyorekebishwa Mwaka 2000).

1.1 Mamlaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

Ibara ya 143 (2) (c) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, inamtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya ukaguzi wa taarifa za fedha zilizoandaliwa na Maafisa Masuuli wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, taarifa za fedha za Mahakama zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na taarifa za fedha za Bunge na kisha kutoa taarifa ya ukaguzi angalau mara moja kila mwaka. Aidha, Ibara hiyo ya 143 (3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 (kama ilivyorekebishwa mara kwa mara) inatanabaisha kuwa, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kila mtumishi wa Serikali aliyeruhusiwa na yeye, atakuwa na haki ya kuchunguza vitabu, taarifa za akaunti na hati nyinginezo zinazohusika na aina yoyote ya akaunti iliyotajwa katika

Ibara ndogo (2). Aidha, Kanuni ya 88 ya Kanuni za Ukaguzi wa Umma za mwaka 2009 inamtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwasilisha Ripoti Jumuifu ya mwaka, kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kabla au ifikapo tarehe 31 Machi kila mwaka. Taarifa hiyo itawasilishwa Bungeni na Waziri mwenye dhamana, kabla ya kumalizika kwa siku saba (7) tangu kuanza kwa Kikao kilichofuata baada ya Ripoti kuwasilishwa kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

1.2 Majukumu ya Ofisi

Hati ya Majukumu (Presidential Instrument) ya Mwaka 2018 imeainisha majukumu ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kama ifuatavyo:-

a) Kukagua hesabu za Wizara, Mikoa, Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Jiji; Ofisi za Balozi za Tanzania zilizoko nje ya nchi; Wakala za Serikali; Mashirika ya Umma; pamoja na Miradi ya Maendeleo inayogharamiwa na Wafadhili, na kutoa taarifa ya ukaguzi huo Bungeni kuhusu mapato na matumizi ya fedha za Umma;
b) Kujenga, kukuza na kuimarisha utamaduni wa uwajibikaji katika Wizara na Taasisi za Serikali, Mikoa na Halmashauri;
c) Kuhakikisha kwamba, inajiridhisha kuwa upo uwajibikaji wa kutosha katika kusimamia na kudhibiti ipasavyo ukusanyaji wa mapato na matumizi ya Serikali kama inavyoidhinishwa na Bunge; na

d) Kuhakikisha kuwa jamii ya Tanzania inapata faida au tija kutokana na matumizi bora ya fedha za Umma, na mali za Umma zinahifadhiwa, kutunzwa na kulindwa ipasavyo.

1.3 Dira

"Kuwa Taasisi yenye Kuaminika na ya Kisasa katika Ukaguzi wa Umma inayotoa Huduma za Ukaguzi za Viwango vya Juu Zinazoimarisha Imani kwa Umma".

1.4 Dhima

"Kutoa huduma za Ukaguzi zenye Kiwango cha Juu kwa njia za Kisasa zenye Kuimarisha Uwajibikaji na Uwazi katika Usimamizi wa Rasilimali za Umma".

1.5 Misingi ya Uadilifu

- ✓ *Kufanya kazi kwa uhuru na bila upendeleo.*
- ✓ *Kufanya kazi kwa utaalam.*
- ✓ *Kufanya kazi kwa uadilifu.*
- ✓ *Kufanya kazi kwa ubunifu na uvumbuzi.*
- ✓ *Kufanya kazi kwa kuzingatia matokeo.*
- ✓ *Kufanya kazi kwa ushirikiano.*

1.6 Haki ya Mwananchi Kupata Taarifa

Ibara ya 18 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeweka bayana kuwa, taarifa ni haki ya mwananchi. Aidha, Sheria Na. 6 ya Kupata Taarifa ya mwaka 2016 na Sheria ya Huduma ya Vyombo vya Habari ya mwaka 2016 zimeweka utaratibu wa utoaji taarifa kwa misingi ya sheria. Ofisi hutoa Toleo Maalumu kwa ajili ya wananchi ili waweze kupata Taarifa za kikaguzi.

Taarifa za Ukaguzi Kwa mujibu wa kanuni ya 8 (5) ya kanuni za Sheria ya Fedha ya mwaka 2001 (iliyorekebishwa 2004); Wizara, Wakala na Idara za Serikali zina jukumu la kuhakikisha kuwa taarifa kuhusu shughuli na rasilimali za taasisi husika zinatolewa kwa umma. Hivyo, ni wajibu wa Serikali kuandaa taarifa za mapato na matumizi yake kisha kila mwananchi kutafuta taarifa hizo ili kufuatilia utekelezaji wa shughuli za maendeleo nchini.

1.7 Rasilimali za Taifa na Uwajibikaji

Rasilimali za Taifa zinajumuisha fedha, maliasili ya nchi,watu, ardhi na mambo mengine yote yanayohitajika katika uendeshwaji wa Serikali kama ilivyoelezwa katika Ibara ya 27 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (pamoja na marekebisho yake). Kwa mujibu wa muundo, mipaka na mamlaka katika usimamizi wa rasilimali za Taifa kati ya mihimili mitatu ni kama ifuatavyo:

1.7.1 Bunge

Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa niaba ya wananchi lina wajibu wa kuidhinisha na kusimamia mapato na matumizi ya Serikali. Wananchi kupitia wabunge wao wanaweza kutoa maoni yao ya namna ambavyo wangependa Serikali iweze kutatua matatizo yao.

1.7.2 Serikali

Serikali inawajibu wa kukusanya na kutumia rasilimali za Taifa kama zilivyoidhinishwa na Bunge.

Serikali inajumuisha Serikali Kuu, Serikali za Mitaa pamoja na Mashirika na Taasisi za Umma.

1.7.3 Mahakama

Mahakama ina wajibu wa kutafsiri Sheria kwa kusikiliza mashauri yote yanayofikishwa Mahakamani na kutoa hukumu kulingana na sheria za nchi.

SURA YA PILI

2.0 MAELEZO YA JUMLA KUHUSU UKAGUZI NA AINA YA HATI ZA UKAGUZI WA TAARIFA ZA FEDHA

Ni wajibu wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kufanya ukaguzi wa hesabu na kutoa mapendekezo kwa mkaguliwa kuhusu namna ya kuandaa taarifa za hesabu kwa usahihi. Aidha, maoni ya CAG kuhusu usahihi au vinginevyo wa taarifa na nyaraka mbalimbali zilizokaguliwa huitwa Hati.

Maoni yanatolewa kwa ufupi kwa kuzingatia sheria na miongozo mbalimbali inayogusa shughuli za kila siku za uendeshaji Taasisi za Umma, Wizara, Mashirika ya Umma na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

2.1 Hati za Ukaguzi

Mwaka huu Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alipitia tafsiri ya Kiswahili ya majina ya hati za Ukaguzi na kuyaboresha kwa baadhi ya hati ili tafsiri hiyo iweze kueleweka vizuri zaidi.

Hivyo, wakati kwa miaka iliyopita, "Adverse Opinion" iliitwa "Hati Isiyoridhisha" na "Disclaimer of Opinion" iliitwa "Hati Mbaya", kuanzia mwaka huu, "Adverse Opinion" inaitwa "Hati Mbaya" na "Disclaimer of Opinion" inaitwa "Kushindwa Kutoa Maoni". Mabadiliko haya yamefanywa ili kuhakikisha kuwa majina mapya yanaakisi kwa usahihi zaidi maana halisi ya hati zinazotolewa.

2.1.1 Hati Inayoridhisha

Aina hii ya hati hutolewa baada ya kujiridhisha kuwa, kutokana na ushahidi uliokusanywa wakati wa ukaguzi, taasisi zilizokaguliwa zimeandaa taarifa zao za fedha kwa usahihi kwa kuzingatia vigezo vyote vinavyotumika vya uandaaji wa taarifa za fedha, yaani Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Taarifa za Fedha katika Sekta ya Umma pamoja na miongozo mingine. Hati hii inajulikana zaidi kwa jina la hati safi, na inatazamiwa kuwa taasisi zote zinajitahidi kupata hati hii kwani inaonesha usimamizi imara wa masuala ya kifedha unaotokana na ufanisi mkubwa wa mfumo wa udhibiti wa ndani.

2.1.2 Hati yenye Shaka

Hati hii hutolewa pale ambapo nimejiridhisha kuwa, kulingana na ushahidi uliopatikana, taarifa za fedha zilizokaguliwa zina makosa makubwa, ama kwa kutozingatia ipasavyo viwango vya kimataifa vya uhasibu pamoja na sera za uhasibu au kulikuwa na kushindwa kukidhi mawanda ya ukaguzi kutokana na kutopatikana kwa nyaraka zote zilizohitajika ili kufanikisha malengo ya ukaguzi lakini makosa hayo hayakuwa na madhara makubwa kiasi cha taarifa hizo kwa ujumla wake kushindwa kutumika katika kufanya maamuzi.

Hii inamaana kuwa makosa hayo au madhara ya kushindwa kupata ushahidi wa kutosha yamejikita kwenye baadhi ya maeneo ya taarifa za fedha lakini sehemu kubwa ya taarifa hizo

zimeandaliwa kwa usahihina zinaonesha hali halisi ya utendaji wa taasisi husika, ndiyo maana hati hii pia hujulikana kama ‘kizuizi cha maoni ya ukaguzi”.

2.1.3 Hati Mbaya

Hati hii hutolewa pale ambapo nimejiridhisha kuwa, kulingana na ushahidi uliopatikana wakati wa ukaguzi, taarifa za fedha zilizokaguliwa zina makosa makubwa na yaliyoathiri sehemu kubwa ya taarifa za fedha, hivyo kupelekea taarifa hizo kutokuwa sahihi. Hii inamaanisha kuwa tofauti na hati yenye shaka, taarifa za fedha zilizoandaliwa zina makosa makubwa yatokanayo na kutokukubaliana au kushindwa kukidhi mawanda na makosa hayo hayajajikita sehemu moja bali yameathiri maeneo mengi katika taarifa za fedha. Hali hii inazifanya taarifa hizo kutokuwa na kigezo cha kuaminika kwa ajili ya watumiaji wa taarifa kufanyia maamuzi.

2.1.4 Kushindwa Kutoa Maoni

Mazingira ya ukaguzi yanaweza kupelekea kushindwa kutoa maoni ya ukaguzi. Hii inatokea pale ambapo nimeshindwa kupata ushahidi wa kutosha au taarifa muhimu ili kufikia malengo ya ukaguzi, na endapo madhara ya kushindwa kupata ushahidi au nyaraka hizo ni makubwa sana. Hivyo, ninaonesha kwenye ripoti yangu ya ukaguzi kuwa kutokana na ukubwa wa madhara yaliyopo au yanayoweza kutokea kutokana na kukosa ushahidi wa kutosha, nimeshindwa kutoa maoni ya ukaguzi.

Kama ilivyo kwa hati mbaya, ninaposhindwa kutoa maoni, maana yake ni kuwa sehemu kubwa ya kiasi kilichoripotiwa kwenye taarifa za fedha hakiaminiki hivyo taarifa za fedha zilizokaguliwa hazifai kwa ajili ya kufanyia maamuzi mbalimbali.

Mchanganuo wa Hati za Ukaguzi Zilizotolewa kwa Mwaka 2019/20



SURA YA TATU

3.0 UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

Sura hii inaelezea mwenendo wa utekelezaji wa mapendekezo mbalimbali yaliyotolewa katika kaguzi za fedha zilizofanyika miaka iliyopita. Hii inajumuisha mapendekezo yaliyotolewa katika ukaguzi wa Serikali Kuu, Serikali za Mitaa, Mashirika ya Umma na Miradi ya Maendeleo. Katika ripoti za Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kwa miaka iliyopita, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali ilitoa mapendekezo mbalimbali yalilenga kuimarisha usimamizi wa rasilimali za umma pamoja na kuboresha ukusanyaji wa mapato.

Ukaguzi uliofanyika pia ulihusisha tathmini ya utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa miaka iliyopita; kati ya mapendekezo 8,740 yaliyotolewa miaka iliyopita, mapendekezo 2,610 sawa na asilimia 30 yametekelezwa kikamilifu. Mapendekezo 2,662 sawa na asilimia 30 utekelezaji wake unaendelea. Aidha, mapendekezo 2,292 sawa na asilimia 26 utekelezaji wake haujaanza; mapendekezo 751 sawa na asilimia 9 yamerudiwa; na mapendekezo 426 sawa na asilimia 5 yamepitwa na wakati. Mchanganuo wa utekelezaji umeainishwa katika Jedwali Na. 3.1 hapo chini.

3.1 Matokeo ya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ya kaguzi za fedha za miaka iliyopita

Ukaguzi uliofanyika pia ulihusisha tathmini ya utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa miaka iliyopita; kati ya mapendekezo 8,740

yaliyotolewa miaka iliyopita, mapendekezo 2,610 sawa na asilimia 30 yametekelezwa kikamilifu. Mapendekezo 2,662 sawa na asilimia 30 utekelezaji wake unaendelea. Aidha, mapendekezo 2,292 sawa na asilimia 26 utekelezaji wake haujaanza; mapendekezo 751 sawa na asilimia 9 yamerudiwa; na mapendekezo 426 sawa na asilimia 5 yamepitwa na wakati. Mchanganuo wa utekelezaji umeainishwa katika Jedwali Na. 3.1 hapo chini.

Jedwali Na 3.1: Hali ya utekelezaji wa mapendekezo kwa miaka iliyopita

Aina ya Ripoti	Idadi ya Mapendekezo	Utekelezaji umekamilika	Utekelezaji unaendelea	Utekelezaji haujafanyika	Mapendekezo Yaliyojirudia	Mapendekezo yaliyopitwa na wakati
Mamlaka ya Serikali za Mitaa	15	6	0	5	4	0
Mashirika ya Umma	116	25	36	52	0	3
Serikali Kuu	5,483	1,508	2,003	1,211	502	259
Miradi ya Maendeleo	3,126	1,071	623	1,024	245	164
Jumla	**8,740**	**2.610**	**2,662**	**2,292**	**751**	**426**
Asilimia	**100**	**30**	**30**	**26**	**9**	**5**

Tathmini inaonesha hali ya utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa miaka iliyopita hairidhishi. Kati ya jumla ya mapendekezo 8,740 yaliyotolewa, ni asilimia 30 tu yametekelezwa kikamilifu. Ukilinganisha utekelezaji wa mapendekezo kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2019 kiwango cha utekelezaji kimepungua kwa silimia 1 kutoka asilimia 31. Tathmini inaonesha kuwa jitihada zaidi zinahitajika ili kutekeleza mapendekezo yote kwa ukamilifu.

SURA YA NNE

4.0 RIPOTI YA UKAGUZI WA HESABU ZA SERIKALI KUU KWA MWAKA 2019/20

4.1 Utangulizi

Sura hii inatoa muhtasari wa matokeo ya taarifa ya Ukaguzi wa Taasisi za Serikali Kuu kwa mwaka wa fedha 2019/20. Taasisi zilizokaguliwa ni 263 ikijumuisha Wizara na Idara za Serikali 66; Vyama vya Siasa 19; Sekretariati za Mikoa 26; Wakala za Serikali 33; Mifuko Maalumu 16; na Taasisi nyingine za Serikali. Kati ya taasisi 263 jumla ya taasisi 260 zilipewa hati mbalimbali za Ukaguzi na taasisi tatu hazikupewa hati za ukaguzi.

Taasisi ambazo hazikupewa hati za ukaguzi ni Vyama viwili vya siasa kwa sababu hazikuandaa na kuwasilisha taarifa zao za fedha kwa ajili ya ukaguzi na Wizara ya Mambo na Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ambayo haikupewa Hati ya Ukaguzi kwasababu ya mlipuko wa ugojwa wa COVID 19 ambapo nchi nyingi zilizuia safari na kufunga mipaka yake. Sehemu kubwa ya Taarifa ya Fedha ya Wizara hii inajumuisha taarifa ya fedha ya Balozi 42 ambazo hazikukaguliwa katika Mwaka wa Fedha 2019/20.



4.2 Matokeo ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali Kuu kwa Mwaka wa Fedha 2019/20

4.2.1 Uandaaji na Utekelezaji wa Bajeti

Katika mwaka wa fedha 2019/20, Serikali ilipanga kukusanya Shilingi bilioni 33,105.41 ikiwa ni ongezeko la Shilingi bilioni 629.46 sawa na asilimia 2 ikilinganishwa na makadirio ya Shilingi bilioni 32,475.95 kwa mwaka wa fedha 2018/19. Katika mwaka wa fedha 2019/20 Serikali ilifanikiwa kukusanya Shilingi bilioni

31,519.49 sawa na asilimia 95 ya Makadirio yaliyopangwa kukusanywa. Hivyo, kiasi cha shilingi bilioni 1,585.92 sawa na asilimia 5 hakikukusanywa. Serikali kwa mwaka wa fedha 2019/20 ilikusanya zaidi kiasi cha Shilingi bilioni 5,702.04 sawa na asilimia 22 ikilinganishwa na makusanyo ya mwaka 2018/19

4.2.2 Makusanyo Katika Mfuko Mkuu

Katika Ukaguzi wa Mfuko Mkuu wa Serikali, mambo yafuatayo yalibainika:

i. Mamlaka za Serikali za Mitaa zilikusanya jumla ya Shilingi bilioni 132.08 na kuzitumia bila kuwasilisha taarifa Mfuko Mkuu wa Serikali ikiwa ni kinyume na Ibara ya 135 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (kama ilivyorekebishwa) ambayo inataka makusanyo yote kwa matumizi ya Serikali kuwasilishwa Mfuko Mkuu wa Serikali;

ii. Jumla ya Shilingi bilioni 2,025.67 zilipelekwa moja kwa moja kwenye miradi ya mendeleo bila taarifa kujumuishwa katika Mfuko Mkuu; na

iii. Bakaa ya fedha kiasi cha Shilingi 1,608,692,098 ilibaki kwa muda mrefu katika akaunti za Amana za wizara tatu[1] pasipo kurejeshwa Mfuko Mkuu ikiwa ni kinyume na Kanuni Na. 133 ya usimamizi wa fedha ya mwaka 2001 inayotaka fedha zote ambazo hazijatumika katika akaunti ya Amana kwa zaidi ya miaka mitano zirudishwe Mfuko Mkuu kwa kibali cha Mhasibu Mkuu.

1 Mahakama ya Tanzania, Wizara ya Maliasili na Utalii na Wizara ya Nishati.

Mapendekezo

Serikali ihakikishe inaimarisha mifumo ya udhibiti wa ndani katika kuongeza uwazi katika makusanyo ikiwa ni pamoja na ufahamu wa umuhimu na uwajibikaji katika kutoa taarifa za makusanyo.

4.2.3 Ukusanyaji na Usimamizi wa mapato

i. Ukaguzi ulibaini kuwapo kwa kesi za muda mrefu katika mamlaka za rufaa za kodi zenye thamani ya shilingi 360,081,657,690,115 za Kitanzania na dola za Kimarekani 181,430,252;

ii. Ukaguzi ulibaini kuwapo kwa pingamizi 44 za kodi zenye thamani ya shilingi 38,780,078,621 ziliyopo katika Idara ya Walipakodi Wakubwa, Idara ya Upelelezi wa kodi na Idara ya Kodi za Ndani ambayo hayajatatuliwa kwa muda unaotakiwa kama ilivyoainishwa katika Mkataba wa Huduma na Mlipa Kodi ya mwaka 2017;

iii. Ukaguzi wa bandari kavu binafsi (ICDs) ulibaini kuwa Makasha (Makontena) 281 yalitolewa chini ya vibali vya dharura pasipo kufanya tathmini ya kodi na kuilipa;

iv. Ukaguzi ulibaini kuwa bidhaa zenye makadirio ya kodi ya forodha ya Shilingi 5,135,360,992 zinazopita Nchini kuelekea nchi jirani kupitia mipaka ya Tunduma, Kasumulu, Rusumo, Kabanga, Mutukula, Namanga, Holili na Kigoma hazikuthibitishwa kutoka nchini; na

v. Ushuru wa forodha na ada ya Shilingi 408,723,375 kwenye lita 3,887,849 za mafuta kutoka nje ya nchi hazikukusanywa kutokana na udhibiti usioridhisha katika usimamizi wa tathmini ya kodi kwenye mfumo wa TANCIS.

Mapendekezo
Serikali ihakikishe inaboresha mamlaka za rufaa za kodi kwa kuziongezea rasilimali ili ziweze kufanyia kazi pingamizi za kodi kwa wakati. Aidha, Serikali iboreshe udhibiti katika mfumo wa TANCIS ili kuziba mianya inayosababisha upotevu wa mapato.

4.2.4 Usimamizi wa Deni la Taifa na Huduma za Jumla

Katika Ukaguzi wa usimamizi wa deni la Taifa, mambo yafuatayo yalibainika:

i. Uchelewaji katika matumizi ya fedha za mikopo kutokana na mipango duni ya matumizi ya fedha za mikopo hiyo kabla ya kusaini mikataba ya ukopaji. Hali hii imesababisha ongezeko la gharama za ukopaji ikiwemo tozo ya kutengewa fedha (Commitment charge);
ii. Kutokuwepo kwa kanzidata (database) ya kitaifa ya miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Serikali kupitia Mikopo. Hali hii inaathiri ufuatiliaji, uratibu na uhamasishaji wa miradi katika ngazi ya taifa;
iii. Majadiliano ya mikopo ya serikali hufanywa bila kuzingatia ubobezi wa watumishi wanaoshiriki katika majadiliano husika. Hii imetokana na kutokuwa na utaratibu rasmi wa

kuteua kiongozi wa mazungumzo na timu mahsusi wenye ujuzi na weledi katika kufanya majadiliano ya mikopo yaletayo unafuu katika ukopaji wa serikali;

iv. Ucheleweshaji wa uandaaji mafao ya wastaafu kwa ajili ya Ukaguzi wa awali kwa hadi miaka 30.

Mapendekezo

i. Serikali ihakikishe inaweka mipango madhubuti ya matumizi ya fedha za mikopo kabla ya kusaini mikataba ili kupunguza gharama za kukopa.
ii. Serikali ihakikishe inaandaa mpango kazi utakaowezesha kukamilisha kwa wakati Mfumo wa Kitaifa wa Usimamizi wa Miradi.
iii. Serikali iweke utaratibu rasmi wa kuteua timu mahsusi yenye ujuzi na weledi wa kufanya majadiliano ya mikopo yaletayo unafuu zaidi kwa Serikali.
iv. Serikali ihakikishe kuwa inashughulikia kwa haraka majalada ya mafao ya watumishi.

4.2.5 Usimamizi wa Rasilimali Watu

Katika usimamizi wa Rasilimali Watu ukaguzi ulibaini mambo yafuatayo:

i. Ilibainika kuwa Serikali ilipanga kuajiri watumishi wapya wapatao 9,522 katika mwaka wa fedha 2019/20. Hata hivyo, Serikali ilipokea kutoka kwa Taasisi mbalimbali maombi ya kuajiri watumishi wapya wapatao 29,805 sawa na 213% ya idadi iliyopangwa na serikali. Kupitia Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, serikali ilitoa vibali vya ajira za Watumishi wapya 9,225 kwa ajili ya Wizara,Idara na Wakala tu ambavyo havikutosheleza mahitaji ya ajira mpya za Watumishi zilizoombwa;

ii. Ukaguzi pia ulibaini kuwa makato ya Shilingi 1,557,988,754.82 ya mishahara ya watumishi kwa ajili ya kuwasilishwa katika taasisi husika ambazo ni Mfuko wa Bima wa Taifa (NHIF), Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) hayakuwasilishwa katika taasisi hizo;
iii. Ukaguzi uliofanywa katika taasisi 80 ulibaini kuwa, madai ya watumishi yanayotokana na malimbikizo ya mishahara pamoja na posho mbalimbali kwa mwaka wa fedha 2019/20 yalikuwa yamefikia Shilingi 331,518,426,304.13 ikilinganishwa na madai ya Shilingi 307,612,008,474.46 ya mwaka 2018/19 hivyo kuwapo kwa ongezeko la madai kwa asilimia 7.8;
iv. Ukaguzi pia ulibaini kuwapo kwa malipo ya mishahara ya Shilingi 59,158,470 kwa watumishi 22 waliokuwa wamekwisha koma utumishi wa umma;

Mapendekezo

Serikali ihakikishe inafanya tathmini ya kina ya mahitaji ya watumishi katika taasisi zake na kuongeza ajira kwenye taasisi hizo ili kuzisaidia kutimiza malengo zilizowekewa. Pia, kuweka mfumo madhubuti utakaohakikisha makato ya mishahara yanawasilishwa kwa taasisi husika kwa wakati.

4.2.6 Wakala za Serikali, Mifuko Maalumu ya Fedha, Mabonde ya Maji, Hospitali za Rufaa za Mikoa na Taasisi Nyingine

Katika ukaguzi wa Taasisi tajwa hapo juu mambo yafuatayo yalibainika:

i. Ukaguzi ulibaini kuwa Wakala wa Ndege za Serikali (TGFA) hawakupokea kiasi cha Shilingi 71,482,878,617 kinachojumuisha tozo ya kukodisha ndege na fedha za akiba ya matengenezo ya ndege kutoka kwa ATCL. Hali hii inaweza kusababisha TGFA kushindwa kufanya matengenezo ya ndege kama miongozo ya ndege inavyotaka hivyo kupungua muda wa maisha na utendaji mzuri wa ndege husika;

ii. TGFA ilitumia gharama kubwa ya Shilingi 3,916,377,800 kufanya matengenezo ya ndege tarehe 14 Februari na 26 Aprili 2018. Hata hivyo, ukaguzi uliofanyika tarehe 19 Agosti 2020 ulibaini kuwa ndege hiyo ilikuwa haifanyi kazi na imetelekezwa tangu mwaka 2015. Hali ya kufanya matengenezo kwa ndege ambayo haifanyi kazi inasababisha hasara kwa taifa;

iii. Ukaguzi ulibaini kuwa makusanyo ya kivuko ya jumla ya Shilingi 81,194,650 yaliyokusanywa na TEMESA kuanzia tarehe 1 Julai 2019 hadi tarehe 30 Juni 2020 hayakupelekwa benki na hayakuwepo kwenye himaya ya TEMESA wakati wa ukaguzi tarehe 31 Julai 2020. Hali hii inaashiria kuwa fedha hizi zilitumiwa vibaya katika shughuli zingine;

iv. Ukaguzi ulibaini ubadhirifu wa Shilingi 201,008,694.79 uliomhusisha mtumishi wa TEMESA akishirikiana na watumishi wa benki mojawapo ya biashara, wakitumia

akaunti ya benki ya matumizi ya kawaida na ya maendeleo zilizopo kwenye benki hiyo. Ubadhirifu huu ulihusisha hundi za benki zilizokuwa zimefungwa na kutolewa kwa ajili ya kulipa kodi ya zuio na kodi nyinginezo kwa Kamishna wa Mapato ya Ndani ambapo zilifunguliwa na kutolewa fedha taslimu;

v. Ukaguzi ulibaini kuwa TEMESA ilifanya mauzo ya tiketi za kielektroniki 21,447,004 katika kituo cha feri Magogoni zenye thamani ya Shilingi 5,757,048,150 kwa mwaka wa fedha 2019/20. Hata hivyo ni tiketi 9,122,690 tu zenye thamani ya Shilingi 3,162,931,550 ndizo zilizothibitishwa na mashine (scanned) na kuacha jumla ya tiketi 12,324,314 zenye thamani ya Shilingi 2,594,116,600 ambazo zilitumika bila ya kuthibitishwa na mashine (not scanned). Hali hii inatoa mwanya wa tiketi ambazo zimetumika na hazikuthibitishwa (scanned) katika mfumo kutumika zaidi ya mara moja hivyo kuikosesha Serikali mapato;

vi. Ukaguzi pia ulibaini kuwa miradi ya ujenzi wa barabara chini ya TARURA yenye thamani ya Shilingi 1,959,810,460 imetelekezwa na wakandarasi mbalimbali kabla ya kukamilika huku sababu kuu ikiwa ni kuchelewa kwa malipo ya wakandarasi pamoja na usimamzi usioridhisha wa miradi husika;

vii. Katika ukaguzi wa Mfuko wa Taifa wa Usimamizi wa Maafa ilibainika kuwa Shilingi 4,314,702,035 zilipokelewa kutoka kwa wadau mbalimbali kwa ajili ya kupambana na janga la

COVID 19. Hata hivyo, Mfuko haukuwa umetumia fedha hizi ukisubiria maelekezo kutoka vyombo husika;

Mapendekezo

i. Seikali ihakikishe Shirika la Ndege (ATCL) linakuwa na mkakati madhubuti utakaosaidia kuilipa TGFA gharama iliyobakia ya Shilingi 71,482,878,617.
ii. Serikali ipitie mchakato mzima wa matengenezo ya ndege na kuchukua hatua stahiki kwa wote waliohusika kutumia gharama kubwa kwa matengenezo ya ndege ambayo haifanyi kazi.
iii. Serikali ifanye uchunguzi juu ya ukusanyaji wa mapato katika kivuko cha Magogoni na kuboresha mfumo wa udhibiti wa ndani ili kuziba mianya ya ubadhirifu iliyopo.
iv. Serikali kupitia TARURA ihakikishe Wakandarasi wanalipwa kwa wakati ili wakamilishe miradi kwa muda uliopangwa. Aidha, Serikali ihakikishe inaandaa mpango kazi wa matumizi ya fedha za kupambana na janga la COVID 19 ili kuepuka vihatarishi vinavyoweza kupelekea matumizi mabaya ya fedha hizo.

SURA YA TANO

5.0 MATOKEO YA UKAGUZI WA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA

Sura hii inatoa muhtasari na majumuisho kuhusu kaguzi za taarifa za Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizofanyika katika mwaka wa fedha 2019/2020

Matokeo ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali za Mitaa

Matokeo ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni 2020 ulibaini mapungufu katika maendeo yafuatayo.

Utekeleza wa Bajeti

Ukaguzi umeonesha kuwa Halmashauri 176 zimekusanya jumla ya Shilingi 639,401,151,405 ikilinganishwa na bajeti ya Shilingi 725,633,433,451,671 ikiwa ni asilimia 89 ya bajeti. mchanganuo huu hauhusishi Halmashauri tisa zilizopata hati zenye shaka.

Miamala yenye viashiria vya udanganyifu ya thamani ya Sh. Milioni 614.51

Ukaguzi ulibaini viashiria vya udanganyifu kwenye malipo kwa wadai mbalimbali na makusanyo ya mapato yenye thamani ya Sh. Milioni 614.51 kwenye halmasahuri za wilaya tisa kama inavyooneshwa kwenye Jedwali Na. 1.

Miamala hii imesababishwa na udhaifu katika udhibiti wa ndani wa halmashauri husika hivyo kushindwa kubaini na kuzuia kutokea kwake.

Mikopo iliyopindukia kwa watumishi bila kudhibitiwa na mamlaka za serikali za mitaa

Watumishi 3,038 katika Mamlaka 35 za Serikali za Mitaa walikuwa wakipokea chini ya 1/3 ya mishahara yao kitendo kinachoathiri utendaji wa watumishi hao. Hali hii ilichangiwa na ulipaji wa madeni la Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ambapo Bodi ya Mikopo ilikikua ikitoza asilimia 18 ya mshahara wa mtumishi aliyenufaika na mkopo huo.

Aidha, tumegundua watumishi nane (8) katika Mamlaka 6 za Serikali za Mitaa ambao hawapati kiasi chochote cha mshahara kila mwisho wa mwezi kutokana na mikopo iliyopita kiwango. Mamlaka hizo na idadi ya watumishi ni H/Jiji Arusha (1), H/W Kiteto (1), H/W Njombe (1), H/M Temeke (1), H/W Rombo (3) na H/W Same (1). Hali hii inaweza kusababisha watumishi hao kutumia muda wa kazi kufanya shughuli binafsi ili kujipatia kipato hivyo kuathiri utoaji wa huduma kwa jamii.

Miradi ambayo haikukamilika Sh. bilioni 184

Nilibaini miradi mbalimbali isiyokamilika yenye thamani ya Shilingi bilioni 184 katika Halmashauri 101 hivyo kuchelewesha huduma kwa jamii iliyokusudiwa. Hii ilisababishwa na kutolewa kwa fedha pungufu za miradi, usimamizi na ufuatiliaji usioridhisha wa menejimenti za Halmashauri, kutelekezwa kwa miradi kwa muda mrefu pamoja na ushiriki usiotosheleza wa jamii katika utekelezaji wa shughuli za miradi.

Miradi ambayo haikutekelezwa Sh. bilioni 14.90

Miradi yenye thamani ya Sh. bilioni 10.55 katika Mamlaka 26 za Serikali za Mitaa haikutekelezwa kutokana na ucheleweshwaji wa fedha ambazo

zilitolewa mwisho wa mwaka wa fedha kati ya tarehe 26 na 30 Juni 2020. Aidha, kazi zilizopangwa kutekelezwa kwenye Mamlaka sita za Serikali za Mitaa zenye thamani ya Sh. bilioni 4.35 hazikutekelezwa kwa sababu fedha za kutekeleza kazi hizo hazikutolewa na Hazina. Hali hii inasababisha Mamlaka za Serikali za Mitaa kushindwa kutoa huduma kwa wananchi kwenye miradi yenye thamani ya Shilingi bilioni 14.90 (Sh. bilioni 10.55 na Sh. bilioni 4.35).

Miradi iliyokamilika lakini haitumiki Sh. bilioni 18.33

Miradi yenye thamani ya Sh. bilioni 18.33 katika Mamlaka 40 za Serikali za Mitaa ilikamilika lakini haikuwa ikitumika kama ilivyokusudiwa. Hivyo, kuna hatari miradi hiyo ikaharibika bila jamii kunufaika.

Halmashauri kutochangia Sh. bilioni 5.72 za asilimia 10 ya vyanzo vya ndani kwenda Mfuko wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu

Mamlaka 82 za Serikali za Mitaa hazikuchangia Mfuko wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu jumla ya Sh. bilioni 5.72 kutoka kwenye mapato ya ndani kinyume na Kifungu cha 37(A) cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa (iliyorekebishwa mwaka 2019).

Mikopo iliyotolewa kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu isiyorejeshwa Sh. bilioni 27.79

Nilibaini mikopo iliyotolewa kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kiasi cha Sh. bilioni 27.79 katika Mamlaka 130 za Serikali za Mitaa bado hazikurejeshwa hadi kufikia tarehe 30 Juni 2020. Hii ilisababishwa na ufuatiliaji hafifu wa mikopo hiyo.

Hasara ya Sh. milioni 186.32 kutokana na udanganyifu wa nukuu za gharama katika nyongeza ya mkataba

Nilitilia shaka ongezeko la gharama lisilo la kawaida katika kazi ya nyongeza ya mkataba Na. LGA/098/HQ/2018/19/W/10 wa ujenzi wa Stendi ya Kisasa ya Mabasi ya Katumba Azimio (Halmashauri ya Katavi) kiasi cha Sh. 186.32 ambalo liliidhinishwa na bodi ya zabuni mnamo tarehe 27 Novemba 2019. Mkataba ulianza tarehe 24 Aprili 2019 na ilikuwa imepita miezi saba hadi tarehe ya kuidhinishwa nyongeza hiyo, ambapo kwa muda huo kupita ni jambo ambalo lingeweza kuathiri gharama za nyongeza ya kazi. Hata hivyo, ulinganifu wa bei katika mkataba wa awali na bei zile zilizo kwenye kazi ya nyongeza ulionesha ongezeko kubwa la bei hadi kufikia asilimia 2,567.

Uchambuzi kulingana na kiwango cha wastani cha mfumuko wa bei uliotolewa na Benki Kuu ya Tanzania katika kipindi hicho ulionesha kwamba bei haiwezi kupanda maradufu katika kazi za nyongeza ikilinganishwa na bei halisi ya mkataba ndani ya kipindi cha miezi 7, hali hii ilionesha udanganyifu wa wazi uliolenga kusababisha hasara. Pia, menejimenti haikutunza kumbukumbu zozote zilizotumika kujiridhisha na bei hizo kubwa kupindukia kabla ya kuweka saini kati yake na mkandarasi.

Malipo ya bidhaa, kazi au huduma zenye thamani ya Sh. bilioni 1.56 ambazo hazikupokelewa. Kinyume na Kanuni iliyotajwa hapo juu, nilibaini kuwa halmashauri 24 zililipa Sh. bilioni 1.56 kwa manunuzi ya bidhaa, lakini bidhaa hizo hazikuwa zimepokelewa na halmashauri husika. Orodha ya halmashauri na thamani ya bidhaa ambazo hazikupokelewa zinaoneshwa kwenye Jedwali Na. 3.

Mikataba yenye thamani ya Sh. bilioni 25.6 haikufanyiwa upekuzi wa kisheria

Mikataba minne katika Mamlaka tatu za Serikali za Mitaa haikufanyiwa upekuzi na mikataba miwili katika Halmashauri ya Mji Makambako na Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe ilipekuliwa baada ya mwajiri kukubali ofa ya wakandarasi. Mikataba hiyo yenye jumla ya thamani ya Sh. bilioni 25.6 imeainishwa katika Jedwali Na. 4.

Kutofanya upekuzi wa mikataba kunaziweka halmashauri katika hatari za kisheria na kunaweza kuhatarisha thamani ya fedha kwa miradi hiyo. Aidha, barua za kukubali ofa ni sehemu ya mikataba hivyo lazima ifanyiwe upekuzi wa kisheria kabla ya kukubali ofa hizo.

Malipo ya Sh. bilioni 5.54 yasiyoambatishwa risiti za kielekitroniki

Halmashauri 58 zilishindwa kuwasilisha risiti za kielekitroniki baada ya kuzitaka kuonesha risiti za manunuzi yenye jumla ya Sh. bilioni 5.54 kama inavyoainishwa kwenye Jedwali Na. 5. Tabia hii inachochea wafanyabiashara kukwepa kodi na kupelekea ukusanyaji mdogo wa mapato ya Serikali.

Malipo yasiyostahili Sh. bilioni 2.09

Nilibaini kuwa Halmashauri 45 zimetumia jumla ya Sh. bilioni 2.09 isivyostahili kulipa shughuli mbalimbali bila kuzingatia sheria na kanuni mbalimbali. Matumizi hayo ni pamoja na malipo ya posho yaliyozidi, malipo ya vibarua bila mikataba, malipo yasiyozingatia viwango maalumu vya posho na malipo yenye viambatisho vyenye shaka. Matumizi haya yanaathiri utekelezaji wa shughuli za Serikali za Mitaa.

Kodi ya zuio ya thamani ya Sh. milioni 761.75 haikuwasilishwa TRA

Nilibaini malipo kwa wauzaji wa bidhaa kwa halmashauri 25 hayakukatwa kodi ya zuio ya jumla ya Sh. milioni 223.60. Pia, kiasi cha Sh. milioni 538.15 cha kodi ya zuio iliyokusanywa na halmashauri 17 hakikuwasilishwa katika Mamlaka ya Mapato Tanzania. Jedwali Na. 6 linafafanua zaidi.

Kutosimikwa Kwa mfumo wa GoT-HOMIS kwenye hospitali, vituo vya afya na zahanati

Vituo vya afya na zahanati 1,439 katika Mamlaka 58 za Serikali za Mitaa hazikusimikwa mfumo wa kielektroniki wa usimamizi na uendeshaji wa huduma za afya kwenye hospitali, vituo vya afya na zahanati (GoT-HOMIS), hali iliyopelekea makusanyo ya mapato kufanyika nje ya mfumo hivyo kutoa mianya ya upotevu wa mapato.

Mapato yanayokusanywa katika vituo vya afya na zahanati ambazo hazijawekewa mfumo wa kukusanyia mapato yanaweza kutumika vibaya bila kugundulika na uongozi wa vituo husika.

Mapungufu yaliyobainika katika usimamizi wa mashine za kukusanyia mapato (POS)

Mashine za kukusanyia mapato 613 katika mamlaka 19 za serikali za mitaa zilikuwa zimeharibika na hazitumiki, na hakuna hatua zilizochukuliwa na mamlaka husika ili kuzitengeneza au kuziondoa kwenye mfumo wa mapato. Pia, mamlaka hizo hazikufanya uhakiki wa mapato yaliyokusanywa na mashine zilizoharibika ili kujiridhisha kama fedha zote zilizokusanywa na mashine hizo zilipelekwa benki.

Halikadhalika taarifa ishara 'dashboard' ya mfumo wa kukusanyia mapato katika Halmashauri 54 ilionesha kuwa mashine 1,469 (Jedwali Na. 7) zilikuwa nje ya mtandao kati ya siku 2 hadi siku 1,570. Kitendo hiki kinatoa mwanya wa upotevu wa fedha zinazokusanywa na mashine hizo.

Mapato yaliyokusanywa lakini hayakupelekwa benki Sh. bilioni 18.77

Mamlaka 135 za Serikali za Mitaa zilikusanya Sh. bilioni 18.77 (Jedwali Na. 8) kutoka vyanzo mbalimbali, hata hivyo hakuna ushahidi unaoonesha kuwa kiasi hicho kiliwasilishwa benki. Hii inaashiria usimamizi hafifu wa mapato.

Mapato yaliyokusanywa nje ya mfumo wa LGRCIS Sh. bilioni 1.34

Nilipitia taarifa mbalimbali za ukusanyaji wa mapato katika Halmashauri 22 na kubaini kiasi cha Sh. bilioni 1.34 kilikusanywa kwenye leseni za biashara na vyanzo vinginevyo nje ya mfumo wa mapato. Hali hii inatoa mianya ya upotevu wa mapato. (Jedwali.Na. 9). Mapato yanayokusanywa nje ya mfumo yanaweza kutumiwa vibaya na wakusanyaji bila kugundulika.

Miamala ya Sh. bilioni 4.79 iliyofutwa kwenye mfumo wa mapato bila kuwa na viambatisho muhimu

Miamala ya mapato inayofikia kiasi cha Sh. bilioni 4.79 katika halmashauri 35 ilifutwa kwenye mfumo wa mapato ili kurekebisha taarifa bila kuambatishwa nyaraka muhimu za marekebisho hayo; wakati mwingine marekebisho hayo hayakuidhinishwa na Mwekahazina au Afisa Masuuli kama inavyooneshwa katika Jedwali Na. 10.

Miamala inayofutwa au kurekebishwa bila kuwepo viambatisho kunaweza kupelekea matumizi mabaya ya mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mapato ambayo hayakukusanywa kutoka kwenye vyanzo mbalimbali Sh. bilioni 30.86

Nilipitia taarifa mbalimbali za mapato zinazotokana na mfumo wa mapato (LGRCIS) na kubaini kuwa Sh. bilioni 30.86 hazikukusanywa katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa 124 kutokana na mauzo ya viwanja, ukodishaji wa vibanda, leseni za biashara, leseni za vileo na vyanzo vingine. Hali hii inaonesha kuwa Halmashauri hazikuwa na ufanisi wa ukusanyaji mapato.

Mapato ya Sh. milioni 179.54 yaliyokusanywa na kutumika kabla ya kupelekwa benki

Halmashauri 4 zilitumia kiasi cha Sh. milioni 179.54 kama marejesho ya fedha zilizotumika kwa shughuli mbalimbali kabla hazijapelekwa benki. Kutumia fedha za mapato ya ndani kabla ya kupeleka benki kunaongeza uwezekano wa fedha hizo kutumika kwa shughuli zisizokusudiwa na hivyo kuongeza hatari ya matumizi mabaya ya fedha za umma. Orodha ya halmashauri zilizotumia fedha kabla ya kupelekwa benki ipo kwenye Jedwali Na. 11.

Mapato ya Sh. Bilioni 2.35 yaliyokusanywa na mawakala hayakuwasilishwa Serikalini

Kiasi cha Sh. Bilioni 2.35 zilizokusanywa na mawakala mbalimbali katika halmashauri 18 hakikuwasilishwa kwenye mamlaka hizo. Kitendo hiki kinaashiria ubadhirifu wa mapato hayo. Jedwali Na. 12 linaainisha halmashauri ambazo mawakala wake hawakuwasilisha fedha Serikalini.

Fedha za mapato ya vyanzo vya ndani Sh. bilioni 33.96 hazikupelekwa kwenye miradi ya maendeleo

Mamlaka 95 za Serikali za Mitaa zilikusanya mapato ya ndani kiasi cha Sh. bilioni 200.99, hivyo jumla ya Sh. bilioni 93.22 (sawa na asilimia 40 hadi 60) zilipaswa kupelekwa kwa ajili ya fedha za miradi ya maendeleo. Hata hivyo, kiasi cha Sh. bilioni 59.26 ndicho kilichohamishiwa kwenye akaunti za maendeleo kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo na kuacha kiasi cha Sh. bilioni 33.96 ambazo hazikupelekwa kwenye miradi ya maendeleo.

Mamlaka tatu za Serikali za Mitaa hazikuweza kabisa kupeleka fedha za mapato ya ndani kwenye miradi ya maendeleo kwa asilimia 100 na Mamlaka nyingine 41 kati ya 95 zilipeleka fedha za mapato ya ndani kwenye miradi ya maendeleo chini ya asilimia 50.

Mashauri dhidi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa yenye jumla ya Sh. bilioni 123.97 na madai ya halmashauri dhidi ya watoa huduma yaliyoko mahakamani kiasi cha Sh. bilioni 13.40

Mamlaka 117 za Serikali za Mitaa kati ya 185 zilikuwa zinadaiwa kutokana na mashauri yaliyo mahakamani yenye thamani ya Sh. bilioni 123.97; na Mamlaka 60 za Serikali za Mitaa zilikuwa na mashauri ya madai mahakamani yenye jumla ya Sh. bilioni 13.40 dhidi ya wadau wake. Madeni tarajiwa yanaweza kuleta athari kubwa kwenye rasilimali fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa, kama vile gharama za uendeshaji wa mashauri na hatari ya kulipa kiwango kikubwa cha pesa baadaye kutokana na halmashauri kushindwa kesi. Hali hiyo ikitokea inaweza kuathiri utoaji endelevu wa huduma za jamii.

Mapungufu kuhusu utendaji wa vitengo vya ukaguzi wa ndani

Vitengo vya ukaguzi wa ndani katika Mamlaka 40 za Serikali za Mitaa havikuwa na vitendeakazi muhimu kama vile kompyuta, kamera, printa na gari la kitengo kwa ajili ya kutembelea miradi ya maendeleo. Katika baadhi ya halmashauri, vitengo vya ukaguzi wa ndani havikuwa na ofisi. Aidha, katika Mamlaka 40 za Serikali za Mitaa baadhi ya shughuli zilizopangwa kama vile ukaguzi wa fedha za elimu zilizopokelewa mashuleni, miradi inayotekelezwa kwa kutumia wataalamu wa ndani (force account), na fedha zilizopokelewa na kutumika kwenye vituo vya afya hazikukaguliwa kutokana na upungufu wa watumishi na bajeti isiyotosheleza. Vilevile, katika Mamlaka 31 za Serikali za Mitaa wakaguzi wa ndani hawana uelewa wa mifumo mbalimbali inayotumika katika mamlaka hizo hivyo kuwawia ngumu kukagua vizuri mifumo hiyo.

Makato ya Mishahara ya Sh. bilioni 5.08 ambayo hayajawasilishwa kwenye taasisi husika

Nilibaini kuwa Mamlaka 46 za Serikali za Mitaa zilishindwa kuwasilisha jumla ya Sh. bilioni 5.08 katika taasisi husika. Miongoni mwa fedha ambazo hazikuhamishwa ni Sh. bilioni 3.92 za mifuko ya hifadhi ya jamii. Hali hii imepelekea Serikali kupata hasara ya kulipa riba inayofikia kiasi cha Sh. bilion 2.76 katika Mamlaka 7 za Serikali za Mitaa. Jedwali Na. 13 linaonesha muhtasari wa kiasi ambacho hakijawasilishwa kwenye taasisi husika hadi kufikia tarehe 30 Juni 2020.

Mikopo ya mshahara ya thamani ya Sh. milioni 95.57 kwa watumishi haikurejeshwa

Mamlaka nne za Serikali za Mitaa hazikukusanya marejesho ya mikopo ya mishahara yenye jumla ya Sh. milioni 95.57 kama inavyoainishwa kwenye Jedwali Na. 14. Hii inaashiria kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa hazina mifumo madhubuti ya kutoa na kurejesha mikopo ya mishahara inayotolewa kwa watumishi.

Ucheleweshaji wa nyongeza ya mishahara na kupandisha watumishi madaraja

Nilipitia mafaili ya watumishi pamoja na Mfumo wa LAWSON wenye taarifa mbalimbali za watumishi na kubaini watumishi 7,992 katika Mamlaka 14 za Serikali za Mitaa hawakupandishwa madaraja ingawa walikuwa na sifa kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma kama inavyoonekana kwenye Jedwali 15. Hali hii inachangia utendaji duni katika kutoa huduma kwa wananchi.

Malipo yasiyostahiki ya Sh. milioni 563.64 wakati wa mchakato wa manunuzi

Wakati wa utekelezaji wa jukumu langu la kikatiba, niliokoa jumla ya Sh. milioni 563.64 zisipotee au kutumika vibaya na wazabuni na maofisa wa serikali wasio waaminifu.

Muhtasari wa malipo yenye makosa na kiasi kilichookolewa umeoneshwa kwenye Jedwali Na. 16.

Malipo ya awali kutorejeshwa baada ya mkataba kuvunjika Sh. 44,114,375

Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro iliingia mkataba Na. LGA/079/2018-2019/HQ/W/08 na Mkandarasi M/S Fast Construction Co Ltd. kwa ajili ya ujenzi wa stendi ya mabasi ya Kaloleni uliosainiwa tarehe 18/10/2019 na kazi za ujenzi zilitarajiwa kukamilika ndani ya miezi minne. Hata hivyo, mkandarasi alishindwa kutekeleza kazi za ujenzi kulingana na makubaliano na hivyo kupelekea kuvunjika kwa mkataba tarehe 19 Februari 2020 wakati mkandarasi akiwa tayari ameshalipwa malipo ya awali ya jumla ya Sh. 108,714,375. Hadi ukaguzi unafanyika, kiasi cha Sh. 44,114,375 kilikuwa bado hakijarejeshwa.

Dosari zilizojitokeza zaidi katika manunuzi ya mwaka wa fedha 2019/20

Nimebaini dosari mbalimbali za manunuzi katika mamlaka za Serikali za Mitaa, kati ya dosari hizo, manunuzi yasiyo na ushindani ndio kasoro inayoongoza ambapo halmashauri 57 zilifanya manunuzi ya Sh. bilioni 9.14 bila ya ushindani wa bei. Muhtasari upo kwenye Jedwali Na. 17.

Manunuzi yenye thamani ya Sh. bilioni 5.01 nje ya mpango wa manunuzi wa mwaka

Mamlaka 17 za Serikali za Mitaa zilinunua bidhaa, kazi, na huduma za Sh. bilioni 5.01 nje ya mpango wa manunuzi wa mwaka kama zilivyoanishwa katika Jedwali Na. 18.

Kushindwa kukidhi mawanda ya ukaguzi kutokana na kukosekana kwa kumbukumbu za manunuzi

Nilibaini udhaifu katika utunzaji wa kumbukumbu za manunuzi na usimamizi wa mikataba ambapo majalada ya manunuzi na mikataba yalikosa baadhi ya nyaraka muhimu. Kwa mfano, katika halmashauri sita manunuzi ya Sh. bilioni 3.02 hayakuwa na nyaraka zinazothibitisha manunuzi hayo; hivyo, sikuweza kuthibitisha uhalali wa manunuzi husika. Orodha ya halmashauri hizo imeoneshwa katika Jedwali Na. 19.

Mikataba yenye thamani ya Sh. bilioni 7.88 ambayo haikuhakikiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali/Halmashauri

Katika halmashauri tisa mikataba yenye thamani ya Sh. bilioni 7.88 haikuhakikiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali au Mwanasheria wa halmashauri husika kinyume na Kanuni ya 59 na ya 60 za Kanuni za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2013 (na marekebisho yake ya mwaka 2016).

Malipo ya Sh. bilioni 5.79 yaliyofanywa bila ya vipimo wala kuthibitishwa na wasimamizi wa miradi

Katika Mamlaka 24 za Serikali za Mitaa malipo ya kazi za ujenzi zenye thamani ya Sh. bilioni 5.79 yalifanywa bila vipimo wala uthibitisho wa mhandisi na msimamizi wa mradi husika. Hali hii inaweza kusababisha malipo kwa kazi ambazo hazikufanyika.

Kuanzishwa kwa miradi yenye thamani ya Sh. Bilioni 3.8 bila umiliki wa ardhi na upembuzi yakinifu

Katika Halmashauri ya Wilaya ya Masasi, matanki 11 ya usambazaji wa maji yenye thamani ya Sh. 432,212,850 yalijengwa kwenye ardhi ambayo haikuwa na milki ya kisheria ikimaanisha kuwa upembuzi yakinifu wa kisheria haukufanyika kabla ya mradi kuanza. Aidha, katika Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga nilibaini kuwepo kwa mizozo kutokana na mabadiliko ya eneo la shughuli za kibinadamu kuzunguka eneo la bwawa

kutoka mita 60 hadi 500 wakati wa utekelezaji wa mradi. Hii ilisababishwa na menejimenti ya halmashauri kutofanya upembuzi yakinifu wa kisheria na wa kitaalamu ili kutenganisha eneo la mradi kwa lengo la kuepusha athari za kilimo kwenye bwawa. Maelezo ya mikataba yanaoneshwa kwenye Jedwali Na. 21.

Miradi Iliyoanzishwa Bila Umiliki wa Ardhi na Upembuzi Yakinifu

Kwa maoni yangu, kuanzisha miradi bila upembuzi yakinifu na kukosekana kwa hatimiliki ya eneo la mradi kumesababisha mzozo wa ardhi na kunaweza kusababisha gharama za miradi kuongezeka na hivyo kupoteza fedha za serikali.

Miradi ya ujenzi yenye thamani ya Sh. Bilioni 3.46 haikujumuisha kwenye mpango wa manunuzi ya mwaka

Mikataba miwili yenye thamani ya Sh. bilioni 3.46 haikujumuishwa kwenye mpango wa manunuzi ya mwaka hivyo ilitekelezwa nje ya mpango kama ilivyoanishwa katika Jedwali Na. 22. Utekelezaji wa miradi kwa namna hii unasababisha mchakato mbaya wa manunuzi na matumizi yasiyopangwa. Aidha, unaathiri utekelezaji wa miradi iliyopangwa na kutengewa bajeti.

Miradi ya Sh. bilioni 23.3 ilitekelezwa bila washauri na kusababisha ucheleweshaji wa huduma ya maji kwa jamii

Halmashauri mbili zilitekeleza mikataba mitatu ya Sh. bilioni 23.38. Katika miradi hii, washauri hawakuhusika kuhakiki miundo ya miradi na kusimamia utekelezaji wake. Hali hii ilisababisha kuongezeka kwa muda (miradi ilichukua miezi 19 hadi 30 kutoka miezi 6 hadi 12 iliyopangwa)

wa miradi kwa sababu ya kusimamishwa kwa kazi na kushindwa kukabili mabadiliko ya mawanda, wakati, na matokeo kinyume na maagizo. Orodha ya miradi iliyotekelezwa bila washauri ipo katika Jedwali Na. 23.

Miradi Inayotekelezwa Bila Washauri

Kutekeleza miradi bila washauri kumesimamisha kazi ili kusubiri wataalamu kutoka Wizara ya Maji kwa sababu washauri hawakuwepo wakati wa utekelezaji wa mradi. Vilevile, imechangia kuchelewesha kukamilika kwa miradi kwa zaidi ya miezi 13 na hivyo kuchelewesha huduma ya maji kwa walengwa.

Matumizi yenye thamani ya Sh. bilioni 3.97 yasiyo na viambatisho

Kwa mwaka wa fedha 2019/20, nilibaini matumizi ya jumla ya Sh. bilioni 3.97 katika halmashauri 87 ambayo hayakuwa na viambatisho ipasavyo na kusababisha kutothibitishwa kwa usahihi na uhalisia wa malipo hayo. Suala hili lilijitokeza pia kwenye kaguzi zilizopita. Halmashauri hazijaonesha utayari wa kurekebisha mapungufu haya. Kwa mfano, kwa miaka mitatu mfululizo (2017/18, 2018/19 na 2019/20), halmashauri 26 zimefanya malipo ya Sh. bilioni 3.47 bila kuwa na viambatisho kama inavyooneshwa katika Jedwali Na. 24.

Malipo yasiyostahili ya thamani ya Sh. bilioni 2.09

Ukaguzi wa matumizi kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2020 ulibaini kuwa halmashauri 45 zilitumia Sh. bilioni 2.09 kwa ajili shughuli mbalimbali bila kuzingatia sheria na kanuni mbalimbali. Matumizi yasiyostahiki ni pamoja na posho yaliyozidi kiwango, malipo ya vibarua bila mikataba, na

malipo mengineyo yasiyozingatia viwango maalumu vya posho na malipo yenye viambatisho yenye shaka. Matumizi haya yanaathari utekelezaji wa shughuli za Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Miamala ya Sh. bilioni 36 ya wadaiwa mbalimbali ambayo haijasuluhishwa kwenye mfumo

Nilipitia taarifa mbalimbali zinazotokana na mfumo wa ukusanyaji mapato katika halmashauri 67 na kubaini kwamba, kiasi cha Sh. bilioni 36 kilikuwa hakijawasilishwa na wadaiwa wanaokusanya mapato kwenye vyanzo mbalimbali. Kuwepo kwa mawakala wanaodaiwa ambao hawajawasilisha mapato kutokana na kutofanya usuluhishi ni kinyume na agizo la 29(2) la Randama ya Fedha za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 linalomtaka mwekahazina kufanya usuluhishi kwa wakati. Jedwali Na. 62 linaonesha wadaiwa ambao miamala yao haikusuluhishwa.

Uhamisho wa fedha Sh. milioni 196.43 kutoka kwenye akaunti ya mapato ya ndani kwenda akaunti ya amana bila kuzingatia taratibu

Katika halmashauri 5 nilibaini kwamba kiasi cha Sh. milioni 196.43 kilihamishwa kutoka akaunti ya mapato ya ndani kwenda akaunti ya amana kama Jedwali Na. 26 linavyoonesha.

Mapato ya ndani yaliyohamishiwa na kutumika kwenye akaunti ya amana hayakuwa na vifungu vya kufanyia malipo kwa fedha zinazotokana na mapato ya ndani. Hali hii inapelekea kuonesha matumizi madogo kuliko uhalisia kwenye hesabu za halmashauri husika. Pia, fedha zilizohamishwa

bila kufuata taratibu zinaweza kutumika kwenye shughuli ambazo hazikukusudiwa.

Magari na mali zingine kutofanyiwa matengenezo au kutoondoshwa kwenye halmashauri husika

Ukaguzi wa halmashauri ulibaini jumla ya magari 727, pikipiki 138, na mali zingine 31 kama vile kompyuta na samani zilikuwa hazitumiki, zimetelekezwa, au kutofanyiwa matengenezo kwa muda mrefu bila menejimenti kuonesha juhudi za kuzifanyia matengenezo ili kuzitumia au kuziondoa kwenye taasisi husika.

Thamani ya mali hizo inaweza kushuka na hivyo Serikali kushindwa kunufaika nazo wakati ingeweza kunufaika iwapo halmashauri zingeamua kuzifanyia matengenezo au kuziondoa mapema inavyowezekana.

Hoja hii imekuwa ikijirudia kwenye taarifa zangu zilizopita jambo linaloashiria kuwa kuna juhudi ndogo za halmashauri kutekeleza mapendekezo yangu kama inavyooneshwa kwenye Jedwali Na. 27.

SURA YA SITA

6.0 RIPOTI YA UKAGUZI WA HESABU ZA MASHIRIKA YA UMMA

6.1 Utangulizi

Sura hii ni muhtasari wa majumuisho ya matokeo na mapendekezo katika ukaguzi wa Mashirika ya Umma kwa mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni, 2020. Sura hii imeainisha masuala mbalimbali yanayoathiri utendaji wa Mashirika ya Umma na mapendekezo yaliyotolewa ili kuboresha utendaji na kufanikisha malengo waliyojiwekea.

6.2 Matokeo ya Ukaguzi wa Hesabu za Mashirika ya Umma

Katika ukaguzi wa hesabu za Mashirika ya Umma, mapungufu mbalimbali yalibainika kama ifuatavyo:

6.2.1 Kutofuata viwango vya malipo vilivyoidhinishwa katika utoaji wa huduma

Katika Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), ilibainika kuwa, mamlaka ilitumia viwango vya chini vya ushuru katika tozo za kushusha na kupakia mizigo kwenye meli (Stevedoring) na tozo za kutoa mzigo kutoka kwenye gati hadi kwa mteja (shorehandling) kwa pamoja zilitozwa Dola za Kimarekani 8 badala ya 10; na tozo za maegesho ya meli katika eneo la bandari (Dockage/buoyage) yalitozwa Dola za Kimarekani 10 badala ya 15 kwa uingizaji na usafirishaji wa bidhaa nje. Hii ni kinyume na tozo za bandari zilizopangwa kutumika katika bandari zilizopo katika maziwa zilizotolewa Januari, 2018.

Mapendekezo:

Serikli kupitia TPA ihakikishe kuwa kamati ya kupitia tozo inatekeleza majukumu yake ya ufuatiliaji wa viwango vya tozo na kuwa viwango hivyo vinaidhinishwa na Bodi ya Wakurugenzi kabla ya mabadiliko kutekelezwa.

6.2.2 Udhaifu katika usimamizi na udhibiti wa mapato ya kodi za pango

i. Katika Shirika la Masoko la Kariakoo (KMC), ilibainika usimamizi hafifu wa mapato ya ukodishaji wa pango; Soko lilitakiwa kukusanya Shilingi milioni 597.54 kutoka kwa wapangaji 963 kulingana na taarifa za kitengo cha biashara kwa kiasi cha Shilingi 1,700 kwa mpangaji mmoja kwa siku moja. Lakini zilikusanywa Shilingi milioni 285.22 hivyo, Shilingi milioni 312.32 hazikukusanywa. Hii inaashiria kuwa KMC linapoteza mapato kutokana na usimamizi hafifu kwa wapangaji.

ii. TPA ilikodisha ardhi (Ukanda wa Bandari ya Mtwara) kwa EPZA mwaka 2014, kwa kipindi cha miaka 33, ada ya kukodisha ya miaka kumi ya Dola za Kimarekani milioni 3.6 ilitakiwa kulipwa kabla. EPZA ililipa Dola za Kimarekani milioni 1.51 tu na Dola za Kimarekani milioni 2.09 hazijalipwa. Pia, TPA ilikodisha ardhi (Bandari za Ndumbi) kwa TANCOAL Energy Limited (TEL) mwaka 2012. TEL ilitakiwa kulipa kodi kabla kila robo mwaka, hata hivyo, hadi mwaka 2019/20, TEL haikuwa imelipa kiasi cha Shilingi milioni 745.79 ambazo imelimbikiza tokea mwaka 2012.

iii. Chuo cha Taifa cha Sukari (NSI) kina nyumba 123 za makazi zilizo katika muundo na ukubwa tofauti ambazo ziliingiza mapato ya kodi ya pango ya Shilingi milioni 111.24 kwa mwaka 2019/20. Hata hivyo, ilibainika kutokuwepo kwa mikataba ya upangishaji kati ya NSI na wapangaji 123. Na makusanyo ya mapato yalifanyika bila kutumia ankara za Mfumo wa Kielektroniki wa Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali (GePG), na hakukuwa na viwango vya kodi vilivyoainishwa kwa kila aina ya nyumba. Kitendo hiki kinatoa mianya ya upotevu wa mapato.

Mapendekezo:

Serikali ihakikishe inaimarisha mifumo ya ufuatiliaji na usimamizi wa mikataba na wapangaji pia itoe hati za madai na namba za kulipia (Control Number) kwa malipo yanayotakiwa. Aidha, Serikali iweke viwango vya malipo ya pango pamoja na kuimarisha udhibiti wa makusanyo ya malipo hayo.

6.2.3 Makusanyo ya Mapato Nje ya Mfumo wa Kielektroniki wa Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali (GePG) Shilingi bilioni 7.23

Ilibainika kuwa taasisi sita (6) Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Dawa, Chuo cha Teknolojia Dar es salaam, Shirika la Posta Tanzania, Chuo cha Taifa cha Sukari, Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Morogoro na Bodi ya Kahawa Tanzania zilikusanya mapato yanayofikia Shilingi bilioni 7.12 nje ya mfumo wa GePG kinyume na matakwa ya sheria. Kitendo hiki kinatoa mianya ya upotevu wa mapato.

Mapendekezo:

Serikali ihakikishe mapato yote ya Taasisi na mashirika yaliyobainishwa yanakusanywa kupitia GePG.

6.2.4 Ubadhirifu wa fedha katika Mamlaka ya Bandari Tanzania Shilingi Bilioni 3.93

Ilibainika kuwepo vitendo vya ubadhirifu katika Bandari ya Mwanza na Kigoma. Katika Bandari ya Mwanza, Shilingi bilioni 3.27 zilitolewa katika akaunti ya benki ya TPA iliyopo CRDB kupitia miamala 737. Vitabu vya fedha havikuonesha hati za malipo na pia matumizi ya fedha hizo hayakuoneshwa. Katika Bandari ya Kigoma, Shilingi milioni 655.90 zilitolewa kutoka benki kwa kutumia hundi 30 bila kuwa na hati za malipo kuthibitisha malipo yaliyofanywa, na hundi hazikusajiliwa kwenye daftari la udhibiti wa hundi, na vipande 5 vya hundi havijaonekana katika

daftari la udhibiti wala katika taarifa za benki. Nyaraka kama vitabu vya hundi, hati za uhamishaji fedha na taarifa za bodi ya zabuni hazikutolewa kwa uchunguzi zaidi. Hivyo, uhakiki kamili wa usahihi wa mapato yaliyokusanywa haukufanyika kutokana na kukosekana kwa hati za msingi za mapato.

Mapendekezo:

Serikali kupitia TPA kwa kushirikiana na vyombo vya usalama, ihakikishe kuwa fedha zinapatikana na hatua za kisheria zinachukuliwa dhidi ya watu waliohusika. Aidha, usimamizi wa nyaraka muhimu za kukusanya mapato na kuyapeleka benki unapaswa kuimarisha ili kuepuka upotevu wa mapato.

6.2.5 Malipo ya awali ya muda mrefu bila bidhaa na huduma kupokelewa Shilingi Bilioni 1.31

Ilibainika uwepo wa malipo ya awali yaliyolipwa kwa muda mrefu bila ya bidhaa na huduma kupokelewa. Malipo yalifanywa na Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI), Ukanda wa Kutengeneza Bidhaa za Kuuza Nje ya Nchi (EPZA) na Chuo Kikuu cha Dodoma yenye thamani ya jumla ya Shilingi bilioni 1.31 kwa wazabuni au watoa huduma 11. Malipo haya yalifanyika zaidi ya mwaka mmoja uliopita.

Mapendekezo:

Serikali ihakikishe uongozi wa MOI, EPZA na UDOM unachukua hatua za kisheria na kurejesha malipo ya awali yaliyolipwa muda mrefu bila kuchelewa.

6.2.6 Taasisi zenye wadaiwa sugu zenye thamani ya Shilingi trilioni 1.01

Ukaguzi ulibaini kuwa kati ya Mashirika ya Umma 165 ambayo yalikaguliwa, ilibainika mashirika 66 yana madai ya muda mrefu yanayofikia kiasi cha Shilingi trilioni 1.01 (sawa na asilimia 70) ya madai yote. Aidha, kwa kiasi kikubwa madai hayo yanatokana na huduma mbalimbali zilizotolewa kwa wateja. Pia, ilibainika kuwa asilimia 14 sawa na Shilingi bilioni 203.96 ya madai hayo yameishapendekezwa kufutwa.

Mapendekezo:

Menejimenti za COASCO, MSD, ATCL, Mpanda WSSA na TPA zibuni mbinu ambazo zitaongeza ufanisi katika usimamizi na ukusanyaji wa madeni.

6.2.7 Mashirika ya umma yenye madai sugu Shilingi Bilioni 207.4

Ukaguzi ulibaini kuwepo kwa madai sugu dhidi ya Mashirika mengine ya Umma yenye thamani ya Shilingi bilioni 207.41. Madai haya yanaathiri upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kuendelea kutekeleza miradi iliyopangwa. Pia, ilibainika kuwa madai sugu yaliyo katika Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) ni ya wapangaji waliohama majengo ya NHC zikiwemo Wizara na Taasisi mbalimbali za Serikali bila kulipa madeni yao.

Mapendekezo:

Serikali ihakikishe Taasisi zenye madai sugu zinafuatilia madai hayo na kuhakikisha yanalipwa bila kuchelewa zaidi.

6.2.8 Maofisa kukosa Mamlaka ya Kutoa Baadhi ya Huduma kwa Wawekezaji katika Vituo Vinavyotoa Huduma Mahala Pamoja (One Stop Centre)

Ukaguzi ulibaini katika taarifa ya utendaji ya TIC ya robo ya tatu ya Mwaka 2019/20 kuwa Kituo kilikuwa kinatoa huduma nne (4) tu kati ya huduma 11 zilizopangwa kutolewa. Huduma zilizokuwa zinatolewa ni pamoja na utoaji wa vibali vya makazi, vibali vya kazi, vitambulisho vya taifa na hati za muda za ardhi. Hata hivyo, wafanyakazi waliopo katika vituo vinavyotoa huduma mahala pamoja walikuwa hawana mamlaka ya kutoa vibali kwa huduma zilizobaki ambazo ni utoaji wa leseni ya biashara/ viwanda, utoaji wa huduma za kikodi, usajili wa kampuni, vibali vya mazingira, vibali vya ubora, vibali vya dawa pamoja na vibali vya usalama na afya mahala pa kazi. Aidha, ukaguzi ulibaini ukosefu wa mamlaka ya kutoa vibali hivyo katika vituo vinavyotoa huduma mahala pamoja (One Stop Centre) kwa wawekezaji unaosababisha kuchelewa kushughulikiwa maombi ya wawekezaji.

Mapendekezo:

Serikali ihakikishe mchakato wa mabadiliko ya Sheria ya Uwekezaji unaaza bila kuchelewa ili kutoa mamlaka ya kutoa vibali hivyo katika vituo vinavyotoa huduma mahala pamoja.

6.2.9 Kuchelewa kutoa majibu kwa maombi ya wawekezaji

Ilibainika kuwa TRA ilicheleweshа kutoa majibu ya maombi 37 ya vivutio vya kodi kutoka kwa wawekezaji yanayopitia TIC kwa siku 182 mpaka 675 mpaka kufikia tarehe ya ukaguzi tarehe 15 Disemba 2020. Pia, ilibainika kuwa TIC haikuchukua hatua yoyote kwa mamlaka iliyopewa katika Kifungu Na 16 (4) cha Sheria ya Uwekezaji. Hali hii inaweza kusababisha wawekezaji kupoteza imani na TIC kufuatia utendaji usioridhisha wa taasisi zingine za Serikali.

Mapendekezo:

Serikali kupitia TIC ihakikishe inatekeleza Mamlaka yake kama yalivyoainishwa katika Sheria ya Uwekezaji pamoja na kuhakikisha wawekezaji wanahudumiwa kwa wakati na viwango.

6.2.10 Mwenendo wa uwekezaji wa mitaji katika Kanda Maalumu ya Uwekezaji

i. Ilibainika kushuka kwa uwekezaji wa mitaji mipya katika Kanda Maalumu kwa kipindi cha miaka mitano (5) kuanzia mwaka wa fedha 2015/16 mpaka mwaka 2019/20. Kwa mfano, katika mwaka wa fedha 2019/20 kiasi cha mitaji kilichowekezwa kilikuwa kidogo ukilinganisha na miaka mingine, ambapo idadi ya miradi mipya ilikuwa ni miradi mitano (5) yenye jumla ya kiasi cha mtaji wa Dola za Marekani milioni 59.86.

ii. Pia, ilibainika kuwa EPZA ilikuwa inachelewa kutoa Leseni za Uwekezaji katika Kanda Maalumu za Uwekezaji, kwa mfano, ni

leseni tano (5) tu sawa na asilimia 26 zilizotolewa kati ya leseni 14 zilizoombwa katika mwaka wa fedha 2019/20. Wawekezaji hao 14 ambao hawakupata leseni walipanga kuwekeza jumla ya kiasi cha Dola za Marekani milioni 590.94. Hata hivyo, EPZA ilieleza kuwa kushuka kwa kiasi cha uwekezaji pamoja na mambo mengine kunachangiwa na vibali kwa ajili ya kuwekeza kutoka taasisi zingine za Serikali. Taasisi hizo za Serikali ni pamoja na NEMC, Wizara ya Ardhi, Mamlaka ya Ajira, Uhamiaji na TRA.

Mapendekezo:
Serikali iingilie kati ili kutafuta suluhisho la kushuka kwa idadi ya Miradi mipya pamoja na kuhakikisha Mamlaka zote zenye wajibu wa kuendeleza uwekezaji zinatoa huduma ipasavyo na hatua kali zinachukuliwa kwa wafanyakazi wa mamlaka hizo ambao huchelewa kutoa huduma kwa wawekezaji.

6.2.11 Mwenendo wa uwekezaji katika Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC)

Ukaguzi ulibaini kushuka kwa idadi ya miradi inayosajiliwa na TIC katika kipindi cha miaka mitano (5) kuanzia mwaka 2015/16 mpaka mwaka 2019/20. Kwa mfano idadi ya miradi iliyosajiliwa na kituo mwaka 2015/16 ilikuwa ni 420, wakati katika kipindi cha mwaka 2019/20 ilikuwa ni 219, hivyo idadi hiyo ya miradi katika miaka hii imepungua kwa asilimia 48 hali ambayo inaweza kupunguza uwekezaji na ajira. Pamoja na kushuka

kwa idadi ya miradi, pia ilibainika kushuka kwa kiasi cha mitaji pamoja na idadi ya nafasi za kazi zinazotokana na uwekezaji. Kupungua kwa idadi ya miradi mipya kunatokana na mabadiliko ya Sheria ya Fedha ya mwaka 2015 ambayo iliondoa baadhi ya vivutio vya kodi kwa wawekezaji, kwa mfano kuondoa vivutio vya kodi katika upanuzi wa miradi kutoka katika kundi la miradi inayopaswa kupewa vivutio vya kodi.

Mapendekezo:

Serikali ihakikishe inatafuta suluhisho la kushuka kwa idadi ya miradi mipya pamoja na kuhakikisha Mamlaka zote zenye wajibu wa kuendeleza uwekezaji zinatoa huduma ipasavyo na hatua kali zinachukuliwa kwa wafanyakazi wa mamlaka zinazohusika ambao huchelewesha maamuzi. Aidha, Serikali iangalie uwezekano wa kufanya mabadiliko ya Sheria za uwekezaji ikiwemo Sheria ya Uwekezaji ya Mwaka 1997 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2015 ili kuondoa changamoto kwenye masuala yote yanayohusu uwekezaji.

6.2.12 Mapungufu katika kusimamia Masurufu Shilingi Bilioni 9.40

Ukaguzi ulibaini kuwa mashirika 29 yalikuwa na masurufu yenye thamani ya Shilingi bilioni 9.40 ambayo yalikuwa hayajarejeshwa mpaka mwishoni mwa mwaka yakiwa yamezidi siku 14 baada ya kukamilika kwa kazi husika. Ilibainika kuwa Mashirika hayajaweka mkazo juu ya urejeshaji wa masurufu

ikiwa ni pamoja na kufanya makato kupitia mishahara ya watumishi husika. Masurufu ambayo hayajarejeshwa yanaweza kusababisha hasara ya fedha za umma.

Mapendekezo:
Serikali kwa kushirikiana na Mashirika husika iweke msisitizo katika udhibiti wa masurufu yasiyorejeshwa ili kuhakikisha urejeshwaji unafanyika kwa wakati na hatua stahiki zinachukuliwa dhidi ya ucheleweshwaji ikiwa ni pamoja na kukata masurufu hayo kwenye mishahara ya watumishi husika.

6.2.13 Miamala isiyo na viambatisho yenye thamani ya Shilingi bilioni 4.95

Ilibainika kuwa mashirika tisa (9) ya umma yaliingia gharama zenye jumla ya Shilingi bilioni 4.95 katika kutekeleza shughuli mbalimbali lakini gharama hizo zilikosa vielelezo vya kutosha kuhalalisha malipo hayo. Mapungufu haya yanasababishwa na udhaifu katika udhibiti wa ndani wa taasisi husika katika utunzaji wa nyaraka za malipo yanayofanywa katika kutekeleza majukumu ya taasisi hizo.

Mapendekezo:
Serikali ihakikishe inaimarisha mifumo ya udhibiti wa ndani iliyopo katika kutunza nyaraka muhimu na kuhakikisha kila muamala na malipo una viambatisho ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo yaliyofanywa.

6.2.14 Kutorejesha Mikopo ya NSSF kutoka kwenye SACCOS Shilingi Bilioni 14

Ilibainika kuwa, vyama 14 vilivyokopeshwa na Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF) Shilingi bilioni 14 havifanyi marejesho ya mikopo hivyo deni limeongezeka kufikia Shilingi bilioni 28.8. Hali hii inasababisha hasara kwa NSSF na ukosefu wa fedha za kugharamia kazi zingine.

Mapendekezo:

Serikali kwa kushirikiana na Mfuko wa NSSF iongeze juhudi za upembuzi wa amana za mikopo kabla ya kutoa mikopo ili kujihakikishia kuwa thamani ya amana inakuwa kubwa kuliko mkopo. Pia, Mfuko uendelee kushirikisha vyombo vya dola pale juhudi za ndani za mfuko zinaposhindwa.

6.2.15 Deni la Muda Mrefu la Watumishi wa Mikataba Shilingi Bilioni 2.31

6.2.16Ukaguzi ulibaini kuwa Chuo Kikuu cha Dar es salaam kina deni la muda mrefu wa zaidi ya miaka minne la Shilingi bilioni 2.31 mpaka kufikia tarehe 30 Juni 2020 ikiwa ni malimbikizo ya kiinua mgongo kwa watumishi wake ambao mikataba yao ya kazi iliisha kuanzia mwaka 2016 na miaka ya nyuma. Kiinua mgongo hulipwa na Serikali lakini Chuo kilionesha deni hilo katika vitabu vyake kuwa kinaidai Serikali fedha hizo. Kuendelea kuwa na madeni ya watumishi waliomaliza mikataba yao kwa muda mrefu huleta usumbufu kwa watumishi hao na pia fedha

hupoteza thamani kutokana na kupita kwa muda na hivyo kutokuwa na thamani iliyotarajiwa wakati wa kulipwa.

Mapendekezo:
Serikali kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es salaam ifuatilie kwa karibu ili kuhakikisha kuwa fedha hizo zinapatikana na kulipwa kwa wahusika kwa wakati.

6.2.16 Akaunti za Benki zilizokuwa zinafanya kazi bila ya kuwa katika Taarifa za Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

Ukaguzi ulibaini kuwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kilifanya miamala mbalimbali katika akaunti 21 za Chuo yenye jumla ya Shilingi bilioni 1.5 lakini taarifa za akaunti hazikuripotiwa katika taarifa za fedha za Chuo. Kitendo hiki kinatoa mianya ya matumizi mabaya ya fedha za umma kupitia akaunti hizo.

Mapendekezo:
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kiimarishe usimamizi na udhibiti wa akaunti za benki, na kihakikishe miamala iliyofanyika katika akaunti hizi inahakikiwa na kuchunguzwa uhalali wake.

6.2.17 Hatari ya kutoweka kwa vivutio vya utalii katika eneo la Hifadhi ya Ngorongoro

i. Ilibainika kuwapo kwa athari kubwa za kiikolojia na kimazingira zinazohatarisha kuharibika kwa ikolojia na kutoweka kwa wanyamapori katika Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro

Ngorongoro Conservation Area (NCA). Shughuli za kibinadamu zinazoendelea ndani ya eneo la hifadhi zinaathiri maisha ya wanyamapori na zinaharibu miundombinu ya kiikolojia inayosaidia maisha ya viumbe hai katika eneo hilo. Hadi wakati wa ukaguzi mwezi Septemba 2020, bado hapakuwa na maamuzi ya kusitisha shughuli za kibinadamu ambazo zinaendelea kufifisha maisha ya wanyamapori na mazingira ya eneo la hifadhi.

ii. Pia ilibainika kuwa zaidi ya asilimia 75 ya eneo la Bonde la Ngorongoro na sehemu kubwa ya eneo la Ndutu yametapakaa magugu vamizi. Haya ni maeneo muhimu zaidi kwa malisho na makazi ya wanyamapori katika Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro. Pamoja na juhudi za Wizara ya Maliasili na Utalii kuunda timu ya kufanya mapitio ya matumizi mseto ya Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro tangu mwaka 2018, bado Serikali haijafanya maamuzi juu ya nini kifanyike kunusuru eneo hilo. Endapo hali ya sasa itaendelea hivi, ikolojia ya Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro itaharibiwa na kushindwa kusaidia maisha ya viumbe hai katika eneo, hali inayoweza kuhatarisha hadhi ya Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro katika orodha ya urithi wa dunia.

Mapendekezo:

Serikali ifanye maamuzi na kuchukua hatua za haraka:-

i. Kusimamisha shughuli zote za kibinadamu zinazoharibu mazingira na ikolojia ya Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro na kuwezesha mchakato wa kurejesha hali ya uhifadhi wa mazingira na ikolojia ya eneo hilo;

ii. Kudhibiti idadi ya watu na mifugo ndani ya eneo la hifadhi ili kuhakikisha hakuna uharibifu wa mazingira na ikolojia ya eneo; na

iii. Kutafuta mbinu mbadala za kudhibiti na kuhifadhi Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro ili kuwa endelevu.

SURA YA SABA

7.0 RIPOTI YA UKAGUZI WA HESABU ZA MIRADI YA MAENDELEO

Sura hii inahusu muhtasari wa majumuisho ya matokeo ya ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2020. Miradi ya maendeleo iliyokaguliwa imegawanyika katika sekta saba ambazo ni sekta za Nishati na Madini, Maji, Uchukuzi, Afya, Kilimo, Elimu na Jamii na miradi mingine. Miradi hii inafadhiliwa na Serikali ya Tanzania na Washirika wa Maendeleo. Katika ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni, 2020 yalibainika mapungufu yafuatayo:

7.1 Matokeo ya Ukaguzi

7.1.1 Usimamizi wa Bajeti Usioridhisha Shilingi Bilioni 82.65

i. Ukaguzi ulibaini kuwa Shilingi bilioni 55.85 hazikutolewa kati ya bajeti ya Shilingi bilioni 253.87 (ambazo ni sawa na asilimia 22) kwa miradi 11 kwenda kwa watekelezaji wa miradi 144 ambao wapo katika sekta ya Kilimo, Elimu, Nishati na Madini, Afya, Sekta mchanganyiko (Multi sector), Sekta ya kijamii (Social sector) na Sekta ya Maji.

ii. Aidha, ilibainika kuwa watekelezaji wa miradi 13 wamefanya matumizi ya kiasi cha Shilingi bilioni 26.54 nje ya bajeti na mpango kazi wa mwaka 2019/20, ikiwemo Sekta ya Elimu ambayo ndiyo ilikuwa na kiwango kikubwa cha matumizi yaliyo nje ya bajeti kwa Shilingi bilioni 25.62.

Mapendekezo:

Watekelezaji wa Miradi kwa kuwasiliana na washirika wa Maendeleo pamoja na Serikali ya Tanzania kupitia Hazina wahakikishe wanatoa fedha za kutosha ili kutekeleza miradi kwa wakati kulingana na bajeti zilizopangwa. Aidha, watekelezaji wa miradi kuhakikisha mipango ya shughuli za miradi inaandaliwa kwa usahihi na kuhakikisha shughuli zote zilizopangwa zinatekelezwa kulingana na bajeti iliyoidhinishwa.

7.1.2 Kutokulipwa kwa Madeni ya Wakandarasi Shilingi Bilioni 81.52 na Tozo Ucheleweshaji wa Malipo – Shilingi Bilioni 14.84

Ukaguzi ulibaini kutokulipwa kwa madeni ya wakandarasi yapatayo kiasi cha Shilingi bilioni 81.52 kutoka kwenye miradi inayotekelezwa katika sekta ya elimu na usafirishaji.

Pia, ukaguzi ulibaini kuwa miradi tisa (9) ilikuwa ikidaiwa tozo ya kiasi cha Shilingi bilioni 14.84. Kati ya miradi hiyo, miradi saba iliyopo katika sekta ya usafirishaji iliyokuwa ikidaiwa tozo ya Shilingi bilioni 11.61 kutokana na adhabu ya kuchelewesha malipo ya madai ya wakandarasi. Hii ni kinyume na kifungu na 51.1 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba (GCC) kinachosema kuwa "Mkandarasi anapaswa kulipwa madai yake ya kazi ndani ya siku 28 baada ya hati zake za madai kuthibitishwa na Meneja wa Mradi". Aidha, ilibainika kuwa tozo zenye thamani ya Shilingi bilioni 3.1 za Mradi wa Kusambaza Maji wa Same-Mwanga-Korogwe, na kiasi cha Shilingi bilioni 0.13 kwenye Mradi wa Kimataifa wa Kuunganisha Nishati wa Kenya na Tanzania (KTPIP).

Mapendekezo:

Serikali pamoja na watekelezaji wa miradi wawasiliane na Wizara ya Fedha na Mipango ili itoe fedha za utekelezaji wa miradi kwa wakati kulingana na bajeti iliyoidhinishwa, hii itawawezesha watekelezaji wa miradi kulipa madai ya wakandarasi kwa wakati.

7.1.3 Kuchelewa kwa Malipo ya Motisha na Gharama za Kiutawala Shilingi Bilioni 91.65

Ukaguzi ulibaini kuwa Programu ya Kuimarisha Afya ya Msingi kwa Matokeo inayotekelezwa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto haijafanya malipo ya motisha na gharama za kiutawala, kiasi cha Shilingi bilioni 91.65 hazijalipwa kwa Bohari Kuu ya Madawa (MSD), Ofisi za Makatibu Tawala wa Mikoa, Mamlaka ya Serikali za Mitaa na Taasisi za Afya. Hii ni kinyume na kifungu 1.2 na 3.18 cha Mwongozo wa Utendaji wa Ufadhili Kutokana na Matokeo.

Mapendekezo:

Menejimenti ya Wizara ya Fedha na Mipango, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto kwa pamoja kuhakikisha malipo ya motisha na gharama za kiutawala yanafanyika kwa wakati kwa watekelezaji wa Programu ya mfumo wa Ufadhili kwa Matokeo.

7.1.4 Mkandarasi Kulipwa Shilingi Milioni 704.16 kwa Kazi ambayo Hakuifanya

Ukaguzi ulibaini kuwa Mshauri Elekezi (M/s Sky Architects Consultants) alilipwa jumla ya Shilingi milioni 735.31 kupitia cheti cha malipo namba 3 cha tarehe 14 Desemba 2018 kwa huduma yake kwenye ujenzi wa uboreshaji wa Ofisi za Madini kwenye miji ya Bariadi, Musoma na Bukoba. Aidha, ilibainika kuwa malipo mengine ya kiasi cha Shilingi milioni 704.16 yalifanyika

kwa kutumia cheti cha malipo namba 3 ambacho kilitumika kufanya malipo ya awali kwa huduma ambayo ilikuwa bado haijafanywa na Mshauri Elekezi. Malipo haya kwa kazi ambayo haikufanyika ni kinyume na Kanuni Na. 243 (2) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2013 (zilizorekebishwa mwaka 2016) ambayo inaelekeza kwamba, malipo yafanyike baada ya kuthibitishwa na kujiridhisha kiwango cha kazi iliyofanyika kama itakavyooneshwa na mkataba husika.

Mapendekezo:
Menejimenti ya Wizara ya Madini ihakikishe mhandisi mshauri anarejesha kiasi cha fedha kilicholipwa kwa kazi ambayo haijatekelezwa.

7.1.5 Kukosekana kwa Mpango Mkuu wa Kina wa Jiji (Detailed City Master Plan) Kumepelekea Ongezeko la Gharama ya Shilingi Bilioni 28.05 (Bila VAT) kwenye Mradi wa Miundombinu ya Usafiri wa Mabasi Yaendayo Haraka (BRT)

Ukaguzi ulibaini kutofanyika kwa mapitio ya upembuzi yakinifu ya mradi wa BRT tangu kufanyika kwa upembuzi wa awali mwaka 2015 kutokana na kutokuwapo kwa taarifa zinazohusu miundombinu (kama barabara na reli) kwenye mipango ya Serikali. Hali hii ilisababisha mabadiliko ya makadirio na muundo kwenye awamu ya pili, ilihali mradi ukiwa kwenye hatua ya juu ya utekelezaji kinyume na Kifungu kidogo cha 7

cha kifungu 5.1 cha Mapitio ya Muundo na Huduma za Awali za mkataba kwenye mradi wa BRT, awamu ya pili. Mabadiliko hayo yalisababisha kutengeneza daraja la reli la juu kwenye barabara ya bandari ili kuruhusu reli ya SGR kupita kwa urahisi katika eneo hilo na hivyo kusababisha kuongezeka gharama ya mradi kwa kiasi cha Shilingi bilioni 28.05. Mabadiliko haya yalipitishwa kupitia mabadiliko ya kwanza ya mkataba.

Mapendekezo:

Menejimenti ya Wakala wa Barabara (TANROADS) kwa kushirikiana na Menejimenti ya Mabasi Yaendayo Haraka (DART) iimarishe ushirikiano na taasisi mbalimbali husika wakati wa kuandaa Mpango Mkuu wa Kina wa Jiji ili kuhakikisha kuna ujumuishaji wa kutosha kupunguza mabadiliko ya usanifu na ongezeko la kazi za ziada.

7.1.6 Matatizo ya Ubora Kwenye Tabaka la Zege Lililojengwa Kwenye Njia ya Mabasi Yaendayo Haraka

i. Kwa mujibu wa michoro na miongozo ya viwango vya ubora, tabaka la zege kwa ajili ya njia ya mabasi yaendayo haraka lilitakiwa kuwa na unene wa milimita 220, upana wa mita 3.5 kwa tabaka la saruji la C1 na tabaka lililoboreshwa la udongo kiwango cha G15. Ukaguzi ulibaini kutokuwepo kwa ubora wa barabara kutokana na kuwepo kwa nyufa kati ya kilomita 6.40 hadi 8.91. Hali hii ilisababishwa na usafirishaji duni wa zege kutoka kwenye sehemu inayohusika na uzalishaji hadi

mahali pa kazi na mkandarasi kutotoa kiwango cha kutosha cha udongo wa mfinyanzi na uchafu uliotokana na masalia ya mimea katika mchanga.

ii. Aidha, ilibainika kuwepo na aina za nyufa zilizoenea upana wote wa barabara pasipo kuthibitika ni za aina moja. Vilevile, zilibainika nyufa zilizozama ndani kati ya maungio ya kuruhusu kutanuka. Hata hivyo, ilibainika kwamba, Wakala wa Barabara hakuchukua hatua kali na stahiki dhidi ya mkandarasi licha ya matatizo ya ubora yaliyojitokeza.



Mapendekezo:

Menejimenti ya Wakala wa Barabara inatakiwa:

i. Ihakikishe Mkandarasi anarekebisha sehemu zote zilizobainika kuwa na ubora duni kabla hajaweka tabaka la kudumu la zege;

ii. Ichukue hatua kali kwa mkandarasi kwa kazi zote zilizofanyika chini ya kiwango.

7.1.7 Mapungufu kwenye Menejimenti ya Muda wa Kutekeleza Mradi wa SGR

Tathmini ya maendeleo ya mradi wa SGR imebaini kuwa hadi kufikia Desemba 2020 utekelezaji wa kazi 'Lot 1' upo asilimia 88.39 ikiliganishwa na makisio ya asilimia 95.96, ambapo 'Lot 2' ni asilimia 52.2 ikilinganishwa na makisio ya asilimia 98.7.

Ukaguzi ulibaini kuwepo kwa utekelezaji usioridhisha wa ujenzi wa SGR kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na uchelewaji wa ukusanyaji wa vifaa kwa 'Lot 1 na 2'; uchelewaji wa ujenzi wa maeneo muhimu makuu; na uchelewaji wa kuanza shughuli za usanifu na ujenzi wa kilomita 3 'Port Link'.

Mapendekezo:

Shirika la Reli liongeze juhudi kwenye usimamizi wa mikataba ya Ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR) kwa kutatua changamoto zote za kimkataba ili kuwezesha kufikiwa kwa malengo yaliyopangwa kwa wakati kulingana na matakwa ya mikataba.

7.1.8 Hasara ya Shilingi Milioni 379.34 Kutokana na Kuharibika kwa Miwa Kwenye Shamba la Miwa Mbigiri na Uwezekano wa Kupoteza Thamani ya Fedha Shilingi Milioni 499.93 kwenye Shamba la Miwa Mtibwa.

Ukaguzi ulibaini kuwa, miwa ambayo ilipitiliza muda wake wa kuvunwa kwenye mradi wa shamba la miwa Mbigiri iliharibiwa na kusababisha hasara inayokadiriwa kufikia kiasi cha Shilingi 379,338,245. Miwa hiyo iliharibiwa kutokana na kutokuwapo kwa mashine za kuichakata ambazo zilitakiwa kuwa zimeshasimikwa kufikia Desemba 2020. Kama inavyoainishwa katika Mpango mkakati wa Kampuni Hodhi ya Mkulazi (MHCL) wa mwaka 2019/20 mpaka 2023/24. Aidha, ilibainika kuwa Kampuni Hodhi ya Mkulazi (MHCL) na Kampuni ya Sukari Mtibwa ziliingia makubaliano mnamo tarehe 17 Septemba 2020 kwa ajili ya uvunaji wa miwa iliyopitiliza muda wa kuvunwa. Ilipangwa kuwa miwa hekta 740.43 ivunwe kwa mwaka kwenye msimu wa Septemba 2020 mpaka Februari 2021, lakini MHCL ilifanikiwa kuvuna hekta 318 ambazo ni sawa na 43% ya makadirio ya uvunaji yaliyopangwa hapo awali. Ilibainika kuwa, ifikapo Februari 2021 miwa hii itakuwa na umri wa miezi 30, hivyo itakuwa haifai kuvunwa na inakadiriwa kuweza kusababisha hasara ya Shilingi 499,934,750.

Mapendekezo:

Kampuni Hodhi ya Mkulazi iharakishe ununuzi na usimikaji wa kiwanda cha uzalishaji sukari katika shamba la Mbigiri.

7.1.9 Mapungufu kwenye Uandaaji wa Mpango wa Utekelezaji wa Mradi wa Maji Same-Mwanga na Korogwe

Ukaguzi umebaini kuwa mpango wa utekelezaji wa mradi haukuandaliwa vizuri. Hii ilisababisha mapungufu kwenye utabiri wa mahitaji ya kiwango cha maji, miundombinu ya maji, uandaaji wa makabrasha ya zabuni na taratibu za manunuzi kwa ujumla. Ilibainika kuzidishwa kwa makadirio ya ukuaji wa idadi ya wakazi kwa asilimia 37, ambapo pia iliongeza mahitaji ya maji kwa kiasi cha mililita za ujazo 40,891 (40,891m3). Hii ilitokana na makadirio ya mradi kutokuwa sahihi kwenye idadi ya wakazi wa Wilaya za Same, Mwanga na Korogwe ambapo walikadiriwa kufikia watu 456,930 kufikia mwaka 2038.

Makadirio hayo ni tofauti na yale ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu ambayo ni wakazi 287,989. Makosa hayo yamesababisha kuongezeka kwa gharama za usimikaji wa mabomba na pampu kwa kiasi cha Dola za Kimarekani 5,388,514. Aidha, ilibainika kuwepo kwa tofauti ya mwendo na muda wa kutibu maji, jambo linaloongeza hatari ya maji yanayotibiwa kutokuwa salama. Makadirio yanaonesha kuwa, maji yanatakiwa kutibiwa kwa dakika 20 kwa mwendo wa mita 0.5 kwa sekunde, wakati hali halisi imeonesha kuwa maji yanatibiwa kwa dakika 13.23 kwa mwendo wa mita 0.052 kwa sekunde.

Mapendekezo:

Menejimenti ya Wizara ya Maji ihakikishe inafanya yafuatayo:

i. Ipitie upya makisio yake ya mahitaji ya maji yaendane na idadi ya makadirio ya watu ili kuepuka uwezekano wa kuongeza au kupunguza makadirio ya mahitaji ya pampu na mabomba kwa ajili ya kuondoa uwezekano wa kuongezeka kwa gharama za mradi; na

ii. Ifanye upembuzi wa haraka ili kuunda mtambo wa uhakika wa kutibu maji kwa ajili ya kuzuia uwezekano wa mafuriko kwenye kituo cha awali cha kusukuma maji na kuchakata uzalishaji wa maji safi.

7.1.10 Mapungufu katika kuzingatia Taratibu za Ununuzi kwenye Kutekeleza Mradi wa Maji Same-Mwanga

Ukaguzi ulibaini mapungufu yafuatayo:

i. Makabrasha ya zabuni hajaandaliwa vizuri kutokana na wazabuni kutakiwa kutengeneza bei ya dhamana, baadhi ya vipengele vimerudiwa mara mbili kwenye makadirio ya gharama za vitu, na kukosekana kwa uwazi kwenye makadirio ya vifaa vya awali. Mapungufu haya yote yamepelekea ongezeko la gharama za mkataba kwa kiasi cha Shilingi 4,081,939.

ii. Ukosefu wa kumbukumbu za manunuzi zinazohusiana na wakandarasi na washauri elekezi, kutokufuata taratibu za mikataba, kufanyika marekebisho kwenye nyaraka za zabuni na michoro pasipo kufuata taratibu, pamoja na

kutofuata taratibu za kiununuzi na kimkataba kati ya mradi, wakandarasi na washauri elekezi.

Mapungufu haya yameathiri ubora wa kazi, kusababisha migogoro ya kimkataba, mabadiliko ya kazi za kimkataba, na kuchelewa kumalizika kwa utekelezaji wa mkataba. Mathalani, bei za mabomba (DI pipes) zimepanda kwa kiasi cha Dola za Kimarekani 504,435.92 kutokana na kutokadiriwa vizuri kwenye hatua za awali za kutengeneza makadirio ya zabuni. Pia, ilibainika makosa yaliyofanyika wakati wa uchambuzi wa zabuni pasipo kuwa na sababu zilizothibitishwa. Makosa hayo yalihusisha jumla ya Dola za Marekani 2,020,367, sawa na Shilingi 445,000,000.

Mapendekezo:

Serikali kupitia Wizara ya Maji ifanye yafuatayo:

i. Ihakikishe kwamba makadirio ya kiasi na gharama za vifaa yanapitiwa kwa umakini ili kuepuka uwezekano wa kuzidishwa kwa bei za vifaa; na
ii. Iwasilishe nyaraka za manunuzi kwa ajili uhakiki.

7.1.11 Kuchelewa Kumalizika kwa Muda Mikataba ya Mradi wa Maji wa Same-Mwanga na Korogwe

Ukaguzi umebaini kuwa mikataba miwili inayohusiana na mradi huu (mikataba Na. I na IV) haijakamilishwa ndani ya muda uliokubaliwa kwenye mikataba hiyo; ambapo, mkataba Na. I

ulichelewa kumalizika kwa muda wa siku 1,253 na mkataba Na. IV ulichelewa kumalizika kwa muda wa siku 509 mpaka kufikia Desemba 2020. Ucheleweshaji huu umesababisha gharama za ziada kwenye mkataba katika maeneo ya: gharama za awali na usimamizi - Dola za Kimarekani 2,584,257.17 (sawa na asilimia 43.45 ya gharama ya jumla ya mkataba), usimamizi - Dola za Kimarekani 906,947.44 (sawa na asilimia 210 ya gharama jumla ya mkataba), na gharama za awali Shilingi 1,175,019,439.70 (sawa na asilimia 931%). Aidha, nimebaini kulikuwa na makadirio ya chini ya muda wa usimamizi wa mkataba yaliyosababisha kuongezeka kwa gharama hizo kwa kiasi cha Shilingi 1,770,750,000.

Mapendekezo:
Menejimenti ya Wizara ya Maji iimarishe usimamizi wakati wa kutekeleza mikataba ili kuhakikisha kazi zinazotekelezwa kwenye mkataba zinamalizika ndani ya wakati uliokubalika.

SURA YA NANE

8.0 RIPOTI ZA UKAGUZI WA UFANISI

Sura hii inatoa taarifa ya kaguzi za ufanisi kumi na nne zilizofanyika kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Machi 2021. Madhumuni ya ukaguzi wa ufanisi ni kutoa tathmini ya kiwango ambacho thamani ya fedha yaani uwekevu, tija na ufanisi huzingatiwa na taasisi za Serikali zinapotumia rasilimali katika kutekeleza majukumu yake. Maeneo ya kufanya ukaguzi wa ufanisi hubainishwa kwa kutumia vigezo mbalimbali ikiwemo malalamiko kutoka kwa wananchi au umuhimu wa eneo husika kiuchumi na kijamii. Kwa mwaka huu ripoti za kaguzi za ufanisi zilizowasilishwa bungeni ni kama ifuatavyo

8.1 Ukaguzi wa Ufanisi katika Udhibiti wa Taratibu za Usafi kwenye Masoko ya Bidhaa za Chakula Nchini

Lengo la ukaguzi:

Lengo la ukaguzi huu lilikuwa ni kutathmini iwapo Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kupitia Mamlaka za Serikali za Mitaa imesimamia vya kutosha taratibu na shughuli za usafi katika masoko ya chakula kwa ajili ya kuhakikisha kunakuwa na usalama na upatikanaji wa bidhaa salama za chakula kwa wananchi ili kuzuia magonjwa ya kuambukiza.

Mapungufu yaliyobainika:

i. Ufuatiliaji hafifu wa viwango na udhibiti kwa wafanyabiashara wanaopanga bidhaa za vyakula sakafuni kama mboga na bidhaa

nyingine za vyakula kupelekea hatari kubwa kwa afya za watumiaji. Hali hii inasababishwa na kutozingatia kanda za vyakula na kufuatilia upimaji.

ii. Kutokuwepo kwa ufuatiliaji wa kutosha uliofanywa na Halmashauri, Sekretarieti za Mikoa na TAMISEMI katika mambo yanayohusisha uboreshaji wa usafi katika masoko 25 yaliyotembelewa katika ukaguzi. ilibainika pia, TAMISEMI haikuweza kuweka viashiria vya utendaji vya kutathmini usafi wa masoko.

Mapendekezo:

TAMISEMI ifanye ufuatiliaji wa kutosha katika kuboresha usafi wa masoko ya chakula nchini.

8.2 Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu usajili na utoaji wa vitambulisho vya Taifa

Lengo la ukaguzi:

Lengo la ukaguzi huu lilikuwa ni kupima iwapo Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kupitia Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) imehakikisha Watanzania wenye umri wa miaka 18 na zaidi wamesajiliwa na kupewa Vitambulisho vya Taifa ili kuboresha upatikanaji wa shughuli za Kijamii na Kiuchumi.

Mapungufu yaliyobainika:

Ucheleweshwaji wa upatikaniaji wa vitambulisho vya Taifa kwa wastani wa siku 563 (takribani miezi 18) kwa asilimia 78 ya wananchi tangu

kujiandikisha mpaka kupokea Kitambulisho cha Taifa zaidi ya kiwango kinachotakiwa cha siku 180 tangu mwananchi anapojiandikisha. Hali hii ilitokana na kusuasua kwa uzalishaji wa vitambulisho vya Taifa kutokana na ubovu na kutokutumika kwa mashine za uzalishaji kwa kiwango kilichotarajiwa.

Mapendekezo:
NIDA inapaswa kuwa na mikakati itakayowawezesha wananchi wote wenye vigezo kupata vitambulisho kwa wakati unaotarajiwa.

8.3 Ukaguzi wa Ufanisi Kuhusu Utoaji wa Huduma za Matengenezo ya Magari ya Serikalini

Lengo la ukaguzi:
Lengo la ukaguzi huu lilikuwa ni kutathmini iwapo mfumo wa matengenezo ya magari ya Serikali unafanya kazi ipasavyo na unarahisisha upatikanaji wa huduma za kitaalamu na zenye gharama nafuu.

Mapungufu yaliyobainika:
i. Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Matengenezo ya Magari yanayomilikiwa na Serikali haufanyi kazi ipasavyo kuwezesha upatikanaji wa huduma za matengenezo ya magari zenye tija. Mfumo haukusanyi, hauhifadhi, na hauchakati taarifa kamili zinazowezesha upatikanaji wa huduma za matengenezo ya magari zenye tija na gharama nafuu.

ii. Utekelezaji hafifu wa kazi za utengenezaji wa magari katika maeneo yanayohusu ubora, ufanisi wa kiutendaji na usimamizi wa fedha. Hivyo kuathiri kiwango na kiasi cha ubora wa kazi za matengenezo ya magari na ufanisi katika usimamizi wa fedha ambapo katika mwaka wa fedha 2019/20 takribani Shilingi bilioni 11.3 ya fedha zilizotokana na matengenezo ya magari hazikukusanywa sawa na asilimia 28 ya mapato yote yaliyozalishwa.

Mapendekezo:
TEMESA inapaswa kuimarisha mifumo yake ya uendeshaji ili kuwezesha upatikanaji wa taarifa za matengenezo ya magari ili kuongeza ufanisi katika usimamizi wa viwango vya huduma ya matengenezo na ongezeko la mapato.

8.4 Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Udhibiti wa Mafuriko Nchini

Lengo la ukaguzi:
Lengo la ukaguzi huu lilikuwa kutathmini namna ambavyo Ofisi ya Waziri Mkuu kupitia Idara ya Maafa inaratibu utekelezaji wa hatua muhimu katika kudhibiti athari na hatari zinazotokana na mafuriko nchini.

Mapungufu yaliyobainika:
i. Usimamizi usiojitosheleza katika utekelezaji wa mipango miji yenye kulenga kudhibiti athari zitokanazo na mafuriko katika mamlaka husika za upangaji. Hali hii imejidhihirisha zaidi kwenye Serikali

za Mitaa zilizopo maeneo ya mijini kama Halmashauri za Majiji ya Mwanza na Ilala, Halmashauri za Manispaa ya Tabora na Kinondoni.

ii. Kutokuwepo kwa mifereji ya kutosha kando ya barabara katika halmashauri ya Manispaa ya Tabora, Halmashauri za Wilaya ya Babati, Korogwe, Ruangwa, Kilwa, Kilosa na Halmashauri ya Manispaa ya Nyamagana, Kinondoni na Halmashauri ya Jiji la Ilala. Halmashauri hizi zina mtandao wa barabara za mijini zenye urefu kati ya kilomita 297 mpaka 1,664, lakini ni asilimia 0.5 mpaka 15 ya barabara ndizo zenye mifereji ya maji yenye urefu chini ya kilomita 500.

Mapendekezo:

Ofisi ya Waziri Mkuu kupitia Idara ya Maafa ihakikishe inakuwa na mipango endelevu inayoweza kudhibiti athari zitokanazo na mafuriko

.

8.5 Ukaguzi wa Ufanisi juu ya Ununuzi wa Magari ya Serikali kwa Pamoja na Usambazaji wa Mafuta

Lengo la ukaguzi:

Lengo la Ukaguzi lilikuwa ni kupima kama Wakala wa Huduma za Ununuzi Serikalini (GPSA) imesimamia vya kutosha ununuzi wa magari ya Serikali na usambazaji mafuta kwa namna ambayo ilihakikisha gharama nafuu kwa Serikali.

Mapungufu yaliyobainika:

Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini (GPSA) inauza mafuta kwa Taasisi za Serikali kwa kutumia bei elekezi inayotolewa na Mamlaka

ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) kinyume na ilivyotarajiwa.GPSA iliuza mafuta kwa bei ya juu ya rejareja ya EWURA kama makampuni mengine ya mafuta kwa sababu ya kukosa matanki makubwa ya kutunzia mafuta ambayo yangewezesha GPSA kununua mafuta kwa wingi; badala yake imekuwa ikinunua mafuta kutoka kwa makampuni ya mafuta ya ndani kwa bei za jumla na kuyasambaza kwa Taasisi za Serikali kutumia bei elekezi za EWURA.

Mapendekezo:
GPSA ikishirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango ihakikishe wanakuwa na matanki ya kutunzia mafuta ili kuweza kununua mafuta mengi kwa bei ya jumla na kuuza kwa magari ya umma kwa bei elekezi ya chini ili kuipunguzia Serikali gharama ya mafuta.

8.6 Ukaguzi wa ufanisi katika usimamizi wa mali zilizotelekezwa

Lengo la ukaguzi:
Lengo la ukaguzi lilikuwa kutathmini kama Wizara ya Fedha na Mipango (MoFP) kupitia Idara ya Usimamizi wa Mali za Serikali (GAMD) pamoja na Benki Kuu ya Tanzania (BoT) ilisimamia kwa ufanisi mali zilizotelekezwa ili kuhakikisha Serikali inapata mapato yanayotokana na mali zilizotelekezwa.

Mapungufu yaliyobainika:
i. Benki Kuu ya Tanzania haikuhakikisha kuwa Benki zote za Biashara zilizofanya kazi Tanzania kwa zaidi ya miaka 15 zinawasilisha mali

zilizotelekezwa. Hadi kufikia Juni, 2020 jumla ya Shilingi bilioni 2.5 kutoka benki za kibiashara zilikuwa zimewasilishwa Benki Kuu na benki 3 kati ya 26 (sawa na asilimia 11.5) ya Benki zilizopaswa kufanya mawasilisho hayo, kama ilivyoanishwa na Sheria ya Benki na Taasisi za Kifedha ya mwaka 2006 (BAFIA, 2006).

ii. Kutokana na ukosefu wa mamlaka ya kisheria hadi kufikia Juni 2020, Benki Kuu haikuwa imeondosha au kutumia kiasi chochote cha mali za kifedha zilizoripotiwa cha Shilingi bilioni 12.25. Matokeo yake Serikali haijaweza kutumia kiasi hicho cha fedha zilizowasilishwa kutoka benki za biashara na taasisi za fedha kwa njia ya mtandao wa simu kwa matumizi yenye tija.

Mapendekezo:
BOT ihakikishe inakuwa na miongozo inayoelekeza utambuzi usajili na uendeshaji wa mali zilizotelekezwa na benki za biashara.

8.7 Ukaguzi wa ufanisi juu ya usimamizi wa ubora wa chakula kilichosindikwa Nchini

Lengo la ukaguzi:
Lengo la ukaguzi huo lilikuwa kutathmini na kupendekeza mikakati ya kuboresha uwezo wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS) katika kuhakikisha usalama na ubora wa chakula kilichosindikwa kinachouzwa katika masoko ya Tanzania.

Mapungufu yaliyobainika:

i. TBS haikufanya ukaguzi wa ubora wa bidhaa za vyakula vilivyosindikwa vilivyopo sokoni vinavyotengenezwa na wasindikaji 23 wa chakula waliotembelewa kuhakikisha viwango vya bidhaa hizo.

ii. Ukosefu wa utaratibu mzuri wa kutambua wasindikaji wa chakula nchini na ucheleweshaji wa utoaji wa leseni ni mojawapo ya sababu za kushindwa kusajili wasindikaji kwa kiwango cha kuridhisha .Shirika limeweza kusajili wasindikaji 251 kati ya 12,121 (sawa na asilimia 2) ya wasindikaji wa vyakula waliopo nchini. Hali hii inaashiria hatari

za kiafya za walaji wa bidhaa zinazozalishwa na wasindikaji hao wasiokuwa na leseni za TBS.

Mapendekezo:
Shirika la Viwango Tanzania (TBS) lihakikishe linakuwa na mipango madhubuti ili kudhibiti ubora wa bidhaa za vyakula.

8.8 Ripoti ya ukaguzi wa ufanisi kuhusu usimamizi wa vituo vya kutolea huduma za afya

Lengo la ukaguzi:
Lengo kuu la ukaguzi huu lilikuwa ni kutathmini kama Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) kupitia Mamlaka za Serikali za Mitaa ilijenga miundombinu ya Vituo vya Kutolea Huduma za Afya (Vituo vya Afya na Hospitali za Wilaya) kwa kuzingatia mahitaji, muda wa ujenzi, gharama na ubora.

Mapungufu yaliyobainika:

i. Vituo 333 kati ya 447 sawa na asilimia 74 ya vituo vya kutolea huduma za afya vilivyojengwa nchini katika mwaka wa fedha 2015/16 hadi 2019/20 vilicheleweshwa kukamilika kwa miezi 12 hadi 40. Pia, Hospitali za Wilaya 67 kati ya 68 (sawa na asilimia 99%) zilizojengwa nchini, zilichelewa kukamilika. Vile vile, ujenzi wa vituo vya kutolea huduma za afya 33 kati ya 35 sawa na asilimia 94 ya vituo vilivyotembelewa ulichelewa kukamilika kwa muda wa miezi 2 hadi 36.

ii. Utaratibu wa kutosha wa kudhibiti ubora wa ujenzi wa vituo vya kutolea huduma za afya vilivyojengwa haukufanywa na OR-TAMISEMI.Hali hii ilithibitishwa na vituo vya afya 34 kati ya 35 ya Vituo vya Huduma za Afya katika Halmashauri za Wilaya 14, ambavyo havikufanyiwa vipimo vya uchunguzi wa ubora wa vifaa vya ujenzi vilivyonunuliwa. Hii imesababishwa na uhaba wa Wahandisi wa Wilaya, Manispaa na Jiji kwa asilimia 75 hivyo kutokuwa na usimamizi wa kutosha wa kazi za ujenzi.

Mapendekezo:
Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) ihakikishe tathmini ya kutosha ya kudhibiti ubora wa ujenzi wa vituo vya afya inafanyika na kuhakikisha vituo hivyo vinakamilika kwa wakati.

8.9 Ukaguzi wa ufanisi kuhusu ufuatiliaji wa miradi iliyotekelezwa kwa njia ya "Force Account" katika Sekta ya Elimu

Lengo la ukaguzi:
Lengo lilikuwa kutathmini kama Wizara ya Fedha na Mipango (MoFP), Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia (MoEST) na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) wanafuatilia vya kutosha manunuzi na usimamizi wa miradi

Mapungufu yaliyobainika:

i. Kulikuwa na ucheleweshaji katika kutekeleza miradi ambapo miradi 10 kati ya 22 iliyokaguliwa haikukamilika kwa wakati.

ii. Vipimo vya kubaini ubora wa vifaa vya ujenzi katika miradi 12 kati ya 17 havikufanyika. Pia, kazi ya kusimamia miradi ilifanywa na Wahandisi wasio na sifa.

iii. Baadhi ya majengo yaliyokamilika hayakutumika kwa madhumuni yaliyokusudiwa kwa mfano vyumba vya madarasa kutumika kama stoo na bwalo kutotumika kabisa.

Hii imetokana na Halmashauri kushindwa kuwajengea uwezo watumishi wake ili kuweza kusimamia miradi inayotekelezwa kwa njia ya “Force Account”.

Mapendekezo:

Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ihakikishe inawajengea uwezo watumishi wake ili waweze kusimamia miradi inayotekelezwa.

8.10 Ukaguzi wa Ufanisi Kuhusu Udhibiti wa Uhamishaji wa Bei ya Mauziano ya Bidhaa au Huduma Baina ya Kampuni zenye Uhusiano (transfer Pricing)

Lengo la ukaguzi:

Lengo la ukaguzi huu lilikuwa kubaini iwapo Wizara ya Fedha na Mipango na Mamlaka ya Mapato Tanzania wanafanya udhibiti wa

kutosha wa uhamishaji wa bei ya mauziano ya bidhaa au huduma baina ya makampuni yenye uhusiano ili kuboresha ukusanyaji wa mapato yatokanayo na kodi.

Mapungufu yaliyobainika:

i. Kasi ya ukaguzi wa udhibiti wa uhamishaji wa bei ya mauziano ya bidhaa au huduma baina ya makampuni yenye uhusiano haiendani na idadi ya makampuni ya kimataifa yanayostahili kukaguliwa. Mamlaka ya mapato ilikuwa na angalau Makampuni 713 kwenye kanzidata yake. Kati ya hayo makampuni 504 yalihudumiwa na Kitengo cha Kodi za Kimataifa. Hata hivyo kati ya hayo, Mamlaka ilifanikiwa kukamilisha kaguzi kwa kampuni 60 tu.

ii. Upungufu wa Rasilimali watu ulipelekea Mamlaka ya Mapato kushindwa kutekeleza majukumu ya udhibiti wa uhamishaji wa bei ya mauziano ya bidhaa au huduma. Kitengo cha Kodi za Kimataifa kilishindwa kukagua makapuni kati ya asilimia 62 hadi 84. Hivyo Serikali inakosa mapato mengi kutokana na kutokaguliwa kwa makampuni hayo.

Mapendekezo:

Wizara ya Fedha na Mipango ihakikishe inasaidia TRA kwa kuwapatia rasilimali za kutosha za fedha na watu ili kuwezesha mamlaka kufanikiwa kukamilisha kaguzi zake.

8.11 Ukaguzi wa ufanisi juu ya usimamizi wa taka za plastiki

Lengo la ukaguzi:
Lengo la ukaguzi huu lilikuwa ni kutathmini kama Serikali imeweza kusimamia kikamilifu udhibiti wa uchafuzi wa mazingira unaotokana na taka za plastiki katika maziwa makuu na bahari.

Mapungufu yaliyobainika:
Halmashauri hazikuweka kwenye mipango yao wala kutekeleza mikakati ya kitaifa ya usimamiaji wa taka ngumu zikiwemo taka za plastiki. Hii imedhihirishwa na kutokuwepo kwa halmashauri iliyofanyia kazi malengo ya kitaifa ya kusimamia taka ngumu hususani katika urejeshwaji wa taka (punguza, tumia tena, kufanya mbolea na urejeshwaji wa nishati).

Mapendekezo:
OR-TAMISEMI inatakiwa iwe na mipango mikakati ikishirikiana na mamlaka za serikali za mitaa kuhakikisha inasimamia taka ngumu.

8.12 Ukaguzi wa ufanisi juu ya utekelezaji wa mradi wa uzalishaji wa sukari Mbigiri

Lengo la ukaguzi:
Lengo la ukaguzi huu lilikuwa ni kutathmini kama usimamizi wa shamba na Kiwanda cha Uzalishaji Sukari vilifanyika kwa kufuata viwango vilivyowekwa vya utekelezaji na thamani ya fedha ilizingatiwa

Mapungufu yaliyobainika:

i. Mbolea na dawa za kuulia wadudu zenye thamani ya Shilingi milioni 241.89 zilitolewa ghalani ila hapakuwa na maelezo ya namna ambavyo mbolea hii ilitumika.

ii. Miwa iliyopita muda wake wa mavuno ilionekana katika vitalu mbalimbali kwenye shamba la Mbigiri ikiwa imeharibika na kupoteza thamani yake ya kiuchumi. Makisio ya hasara iliyotokana na gharama za uzalishaji wa miwa hiyo ni kiasi cha Shilingi milioni 379.34.

iii. Visima vinne (katika shamba la Mbigiri kitalu E3, D2, E4 na F4 vilichimbwa lakini havitumiki kwa sababu havina uwezo wa kutoa maji ya kutosha kwa shughuli za umwagiliaji. Ilibainika kuwa Mkandarasi aliondoka katika eneo la kazi licha ya kuwa alishalipwa Shilingi milioni 81.5 sawa na asilimia kumi 10% ya gharama zilizoainishwa kwenye mkataba.

iv. Kampuni ya Mkulazi ilishindwa kusimika mtambo wa kuchakata sukari kwa wakati na kusababisha benki ya Azania kusitisha kutoa mikopo kwa wakulima wa nje kiasi cha Shilingi bilioni 1.8 ambazo zingewawezesha wakulima hao kukidhi gharama mbalimbali za kuzalisha miwa.

v. Kampuni ya Mkulazi haijasajiliwa tangu kuanzishwa kwake kwa ajili ya Kodi ya Ongezeko la Thamani. Kampuni iliingia mikataba 52 yenye thamani ya Shilingi bilioni 50.28 na mikataba hiyo imejumuisha Kodi ya Ongezeko la Thamani yenye kiasi cha Shilingi bilioni 7.67 katika mwaka wa fedha 2017/18 hadi 2019/20 ambazo zingeweza kutumika kwa shughuli nyingine.

vi. Kampuni Hodhi ya Mkulazi ilimlipa mkandarasi kiasi cha Shilingi milioni 397.02 kama malipo ya maandalizi bila kuwa na vielelezo vya vipengele vilivyolipwa.

Mapendekezo:
Kampuni ya Mkulazi ihakikishe inasimamia uendeshaji wa shamba la sukari kwa kufuata viwango vilivyowekwa na ihakikishe inasajiliwa kwa ajili ya kulipa Kodi ya Ongezeko la Thamani

8.13 Ukaguzi wa ufanisi katika usimamizi wa utoaji wa misamaha ya kodi katika miradi ya uwekezaji

Lengo la ukaguzi:
Lengo la ukaguzi lilikuwa kutathmini kama Wizara ya Fedha na Mipango kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) zinasimamia kikamilifu misamaha ya kodi ili kuboresha manufaa kwa Taifa.

Mapungufu yaliyobainika:

i. TRA na TIC hawakuweza kufanya ufuatiliaji wa misamaha ya kodi iliyotolewa na kusababisha kushindwa kutoa taarifa za upotevu wa mapato uliotokana na misamaha hiyo. Hii imedhihirishwa na TRA kufanya shughuli za ufuatiliaji 2 kati ya 8 zilizopangwa na TIC kufanya shughuli za ufuatiliaji chache kwenye mradi 1 hadi 18 kwa kanda 4 za Kusini, Ziwa, Mashariki na Kati. Hii inaweza kupelekea matumizi mabaya ya misamaha.

ii. Kuwepo kwa ushirikishanaji mdogo wa taarifa za misamaha ya kodi kati ya TRA na TIC. Hii imedhihirishwa na TIC kutokuwa na uwezo wa kuingia kwenye mfumo wa kodi za ushuru wa forodha (TANCIS) ambao ungewawezesha kupata taarifa mbalimbali za wawekezaji ; pia , kutokuwepo kwa mawasiliano ya kutosha baina ya watumishi wa TRA waliopo Ofisi za TIC na wale waliopo kwenye Ofisi za TRA za Forodha. Hivyo kusababisha TRA kurudia kuomba baadhi ya taarifa kwa wawekezaji wakati taarifa hizo zinapatikana kwenye Ofisi ya TIC.

Mapendekezo:
TRA ihakikishe inashirikiana na TIC katika kupata taarifa za wawekezaji na wafanye ufuatiliaji wa kutosha wa misamaha ya kodi iliyotolewa.

SURA YA TISA

9.0 UKAGUZI WA MIFUMO YA TEHAMA

Sura hii inaelezea kwa ufupi baadhi ya mapungufu yaliyobainika katika utengenezaji, uendeshaji, na usimamizi wa mifumo ya TEHAMA katika taasisi na idara za Serikali zilizokaguliwa katika mwaka wa fedha 2019/20. Mdhibiti na Makaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amefanikiwa kufanya ukaguzi wa mifumo ya TEHAMA.

9.1 MATOKEO YA UKAGUZI

9.1.1 Mapungufu katika mfumo wa MUSE

Mapungufu yaliyobainika katika Mfumo wa Ulipaji Serikalini (MUSE):-

i. Utoaji na urudishwaji wa masufuru hurekodiwa na kuripotiwa kabla ya kurekodiwa kwenye hati ya malipo na kukamilika kwa hatua za malipo.

ii. Mfumo hautunzi kumbukumbu za karadha (prepayment) kwenye leja ndogo (sub ledgers).

iii. Uwepo wa bakaa kwenye "control accounts" (suspense accounts na control accounts) ambazo hazikuainishwa kwenye taarifa ya fedha.

iv. Watumiaji wa mfumo (wahasibu) hawawezi kuhakiki miamala wanayofanya kabla ya kutuma miamala kwenye vitabu vya fedha (posting transations in books of account).

v. Mfumo kutofuata muongozo wa kimataifa wa ukaguzi katika sekta za umma (IPSAS), unaoelekeza matumizi kutambulika pindi huduma inapotolewa na si malipo yapofanyika. Usanidi wa mfumo umefanyika katika misingi ya malipo taslimu hivyo kuzuia miamala kufanyika na kurekodiwa endapo hakuna bakaa katika kifungu husika cha matumizi.

Mapungufu haya hupelekea makosa katika taarifa za fedha, yanayosababisha urekebishaji unaohitajika kufanyika nje ya mfumo. Hivyo, kusababisha kupungua kwa ufanisi na usahihi katika uandaaji wa taarifa za fedha.

Mapendekezo:
Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango ihakikishe inayafanyia kazi mapendekezo yaliyotolewa ili kuzuia madhara yaliyobainishwa.

9.1.2 Mapungufu katika taratibu za utengenezaji na ununuzi wa mfumo wa manunuzi ungamanifu wa ki-eletroniki (TANePS) unaondeshwa na Mamlaka ya Manunuzi ya Umma (PPRA).

i. Mamlaka ya Manunuzi ya Umma (PPRA) haina uwezo wa kitaalamu wa kuchukua na kuundesha mfumo kwani mpaka wakati wa ukaguzi huu mnamo Septemba 2020 bado Mamlaka ya Manunuzi ya Umma ilikuwa ikimtegemea mzabuni yaani European Dynamics katika kufanya maboresho ya mfumo.

Hali hii imesababishwa na ushirikishwaji hafifu wa wataalamu wa TEHAMA wa Mamlaka katika kubuni na kutengeneza mfumo kama ilivyohitajika katika mkataba.

ii. Mnunuzi wa mfumo yaani Mamlaka ya Manunuzi ya Umma (PPRA) hajapokea hatimiliki ya mfumo (Intellectual Property), na pia nimebaini kuwa PPRA haijapatiwa umiliki wa "source code" za mfumo ingawa muda wa udhamini "warranty period" kuisha miaka miwili iliyopita kinyume na kifungu GCC 15.4 cha mkataba. Hii imesababisha PPRA kushindwa kufanya maboresho ya mfumo bila kumshirikisha mzabuni.

iii. Kukosekana kwa maelezo ya kina juu ya mafunzo waliyofanyiwa wataalamu wa PPRA kama ilivyoelezwa katika mpango wa usimamizi wa mabadiliko (Change Management Plan – D13), ibara ya 2.4 kuwa "Kutakuwa na mafunzo ya kina kwa wataalamu wa PPRA na wafanyakazi wengine watakaoisaidia Mamlaka ya Manunuzi ya Umma (PPRA) kutekeleza majukumu ya kusimamia uendeshaji wa mfumo wa TANePS.

iv. Mamlaka ya Manunuzi ya Umma (TANePS) haina mpango ulioidhinishwa unaoonesha mkakati wa kuchukua umiliki na uendeshaji wa mfumo kutoka kwa mzabuni.

Mapendekezo:

Mamlaka ya Manunuzi ya Umma (PPRA) iyafanyie kazi mapendekezo yaliyotolewa ili kuzuia madhara yaliyobainishwa

9.1.3 Uwepo wa mifumo mingi inayofanya kazi zinazofanana

Mifumo iliyobainika kufanya kazi zinazofanana kwa mujibu wa ukaguzi wa mwaka wa fedha 2019/20.

i. Wizara ya Ardhi ina mifumo mitatu inayotumika kusimamia shughuli za ardhi: Mifumo hiyo ni MOLIS ambayo inatumika katika Manispaa za Kigamboni, Temeke, na Ilala; MOLIS v3 ambayo inatumika katika mikoa mingine nje ya Dar es salaam; na ILMIS ambayo inatumika katika manispaa za Kinondoni, Ilala, Ubungo, Temeke na Kigamboni.

ii. Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) imetengeneza mifumo kadhaa ili kuboresha shughuli zinazofanywa na wizara hiyo. Hata hivyo nimebaini kwa namna moja au nyingine mifumo hii inafanya kazi zinazofanana au kushabihiana kama inavyoelezwa hapo chini:

(a) **Planrep:** Mfumo unaotumika katika kupanga, kubajeti, kutoa taarifa katika Halmashauri; na **TiMES:** Mfumo wa Ufuatiliaji na tathmini katika Halmashauri (LGAs). Ufuatiliaji na tathmini ni sehemu ya mchakato wa bajeti. Hivyo basi, Planrep ukiwa ni mfumo wa bajeti ulitakiwa kuwa na moduli ya ufuatiliaji na tathmini badala ya kuwa na mfumo tofauti ambao unaongeza gharama za usimamizi na matengenezo.

(b) **Mfumo wa Taarifa za Shule (SIS):** Mfumo unatumika kukusanya takwimu za shule kama vile mahudhurio ya wanafunzi na maendeleo, idadi ya wanafunzi, walimu, na

vitabu; na **mfumo wa Sensa ya Kila mwaka ya shule (ASEC)**: Mfumo unaotumika katika kukusanya takwimu kutoka shule za msingi, sekondari, na elimu ya watu wazima kwa kutumia dodoso maalumu. Mifumo hii miwili tofauti hukusanya takwimu za shule ambazo zinaweza kufanywa na mfumo mmoja.

(c) **IFT-MIS:** Mfumo wa kusimamia uratibu na kuweka kumbukumbu za ufuatiliaji wa matumizi ya fedha katika Halmashauri, na unafuatilia utekelezaji wa mapendekezo na maagizo ya CAG, PPRA na LAAC; na GARI-ITS: Mfumo unasimamiwa na Mkaguzi Mkuu wa Ndani unatumika kufuatilia hali ya utekelezaji wa matokeo ya ukaguzi katika taasisi zote za Serikali pamoja na Halmashauri. Hii ni mifumo miwili tofauti ambayo ina jukumu la kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo ya CAG, PPRA na LAAC katika Halmashauri.

Uwepo wa mifumo tofauti inayotumiwa kutimiza kusudio moja ni matumizi mabovu ya rasilimali, na huongeza ugumu wa usimamizi, matengenezo, na msaada kwa watumiaji.

Mapendekezo:

Taasisi zinazohusika zihakikishe zinafanya majumuisho ya mifumo inayofanya kazi zinazofanana ili kuepusha matumizi mabaya ya rasilimali za umma, na kupunguza gharama za usimamizi wa mifumo Serikalini.

9.1.4 Kushindwa kufuatilia gharama za utengenezaji wa mfumo

Pamoja na mwelekeo chanya unaofuatwa na Serikali katika kuhakikisha utengezaji na uendelezaji wa mifumo ya Serikali unafanywa kwa kutumia wataalamu wetu wa ndani, ili kuhakikisha Serikali inakuwa na udhibiti wa kutosha katika mifumo yake na pia kukwepa gharama kubwa ambazo huenda zingelipwa kwa makampuni binafsi, hata hivyo ukaguzi wa mifumo umebaini mapungufu katika kufuatilia na kuweka kumbukumbu za gharama za utengenezaji za mifumo kama ifuatavyo:

i. Wizara ya Fedha na Mipango ina jumla ya mifumo ya TEHAMA 17 iliyotengenezwa kwa kutumia wataalamu wa ndani lakini gharama zilizotumika katika utengenezaji wa mifumo hazikuweza kupatikana.
ii. Gharama za kutengeneza mfumo wa kieletroniki wa usimamizi wa taarifa za mapato (TeRMIS) wa TARURA hazijulikani kwa sababu ya kukosekana kwa utaratibu mzuri wa ufuatiliaji wa gharama hizo.

Kutokuwepo kwa uwazi wa gharama zilizotumika katika utengenezaji wa mifumo kunaweza kusababisha matumizi mabaya ya fedha za Umma na kushindwa kujua kama kutumia watumishi wa ndani ni nafuu kuliko wakandarasi.

Mapendekezo:

Taasisi zote za umma zenye mifumo ya TEHAMA na zinazotekeleza miradi ya kutengeneza mifumo ya TEHAMA zihakikishe gharama za utengenezaji wa mifumo husika zinabainishwa na taarifa ya gharama hizo kujumishwa katika taarifa za fedha za taasisi husika.

9.1.5 Udhibiti duni dhidi ya shambulio la ransomware

Katika ukaguzi wa usalama wa mifumo uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2019/20 imebainika kuwepo na visa vitatu vya mashambulizi ya kimtandao maarufu "Ransomware". Ransomware ni aina ya programu haribifu ambayo hutumiwa na wadukuzi kwa lengo la kuficha faili za mwathirika na kumtaka alipe kiasi cha fedha kama masharti au kigezo cha kufunguliwa kwa faili zilizofichwa.

Visa hivi vilisababisha kukosekana kwa huduma katika mifumo muhimu ya matumizi kwa masaa 12 katika moja ya taasisi zilizoshambuliwa. Katika kisa cha pili shambulio la ransonmware lilisababisha athari katika shughuli za usimamizi wa rasilimali watu. Shambulio hili lilipelekea taasisi kutoa huduma kwa mikono kwa muda wa miezi miwili. Halikadhalika, katika kisa cha tatu, taasisi iliyopatwa na shambulio la ransomware ilishindwa kuandaa taarifa za fedha (Financial Statements).

Mapendekezo:

Serikali na taasisi zake ihakikishe inafanya jitihada za kulinda, kuzuia, na kupunguza athari za mashambulizi ya kimtandao ikiwemo kuimarisha usalama wa mifumo, mitandao ya taasisi na kutoa elimu ya usalama wa mitandao kwa watumishi.

9.1.6 Changamoto zilizobainika kwenye mfumo wa ukusanyaji wa mapato katika Serikali za Mitaa (LGRCIS)

Tathmini ya ufanisi wa mfumo wa kukusanyia mapato katika halmashauri zote 185 ilibaini changamoto zifuatazo:-

i. Mfumo unaruhusu mlipaji mmoja kuwa na namba za utambulisho zaidi ya moja (payer IDs) na hivyo kusababisha changamoto kwenye ufuatiliaji wa historia ya malipo ya walipaji. Mfumo unatakiwa kuzuia mlipaji mmoja kuwa na namba za utambulisho zaidi ya moja kwa kuhakikisha kila akaunti ya mlipaji inahusishwa na utambulisho binafsi wa mlipaji kama vile namba ya mlipakodi (TIN).

ii. Mfumo wa mapato kuwa na mwingiliano baina ya halmashauri. Kwa nyakati tofauti watumiaji wa mfumo hujikuta wameingia kwenye halmashauri zisizo zao wakati wamesajiliwa kuingia kwenye halmashauri zao tu.

iii. Mfumo wa mapato haujawekwa vyanzo vyote vya mapato kwenye baadhi ya halmashauri kama ada ya matangazo na ushuru wa huduma na kupelekea vyanzo hivi kukusanywa kupitia vyanzo mbalimbali vya mapato (miscellaneous sources) kwenye mfumo.

iv. Mfumo wa mapato hauwezi kuwasiliana moja kwa moja na mfumo wa usimamizi wa fedha (Epicor) bila kuhusisha mtumiaji.

v. Mfumo wa mapato hauna utaratibu rasmi wa kufanya usuluhishi kati ya miamala ya kwenye mashine za kukusanyia mapato (POS) na mapato yaliyopo kwenye mfumo (LGRCIS).

vi. Kukosekana kwa huduma ya kuaminika ya mtandao na kusababisha shughuli za ukusanyaji wa mapato kusimama kwa muda kwenye baadhi ya maeneo. Hii hupelekea taarifa za ukusanyaji wa mapato kutokufika kwa wakati kwenye mfumo wa mapato.

vii. Kutokana na kuwepo changamoto za mtandao mashine za kukusanyia mapato zinaweza kuwa kwenye mtandao lakini hushindwa kupeleka taarifa za kila siku kwenye seva kuu na hivyo kuonekana kuwa zipo nje ya mtandao.

viii. Mfumo wa mapato hautambui miamala ambayo si ya pesa taslimu, hivyo fedha ambazo hazikukusanywa miaka ya nyuma hata kama zilitambuliwa kwenye hesabu za mwisho hutambulika kama mapato ya mwaka ambao pesa hizo hupokelewa. Mfumo wa mapato unatakiwa kuwezeshwa kutambua mapato yanayotambuliwa kwenye hesabu hata kama mapato hayo yanakuwa hayajawasilishwa kwa pesa taslimu ili kuendana na matakwa ya viwango vya kimataifa vya uandaaji wa hesabu za mwisho.

ix. Kwenye baadhi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa watumiaji wa mfumo waliendelea kuwa hai hata kama watumiaji hao

walikoma kuwa watumishi kwenye mamlaka hizo kwa sababu mbalimbali.

x. Mapato yanayokusanywa kutokana na mauzo ya viwanja yanapokelewa nje ya mfumo wa mapato na hivyo kuongeza hatari ya kutumika vibaya bila kugundulika kirahisi na menejimenti ya halmashauri.

xi. Mfumo wa mapato hauwezi kukokotoa tozo au adhabu ambayo mlipaji atatakiwa kulipa kutokana na kutokufuata taratibu na sheria za ukusanyaji wa mapato au uendeshaji wa halmashauri.

Changamoto hizi kwa ujumla zinasababisha upotevu wa mapato ya Serikali, makosa katika taarifa za mapato, kukosekana kwa usiri na uadilifu hivyo kupelekea taarifa za mfumo kuwa shakani, na kutoa mwanya wa kufanya udanganyifu.

Mapendekezo:

Ofisi ya Rais TAMISEMI ihakikishe inayafanyia kazi mapungufu yaliyobainishwa ili kuboresha taarifa za fedha katika mfumo wa LGRCIS na pia kuziba mianya ya ubadhirifu wa fedha za umma.

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali,

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Jengo la Ukaguzi, Mtaa wa Hazina, S.L.P 950,

41104 Dodoma, Tanzania • Simu: +255 (26) 232 1759,

Nukushi: +255 (26) 232 1245

Barua pepe: ocag@nao.go.tz

www.nao.go.tz